**MBARONI** tuhuma kumuua mpenzi kisa deni 5,000/



UKURASA 3

**MBUNGE** aomba ulinzi akidai kutishiwa kifo

UKURASA 5


Soma madarasa yote jirudie nyumbani

BUFE

IJUMAA JUNI 4, 2021 Nipashe BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

AGRI-CONNECT Mradi uliolbua mavuno mapya kahawa, maisha mapya walimaji Nyanda za Juu

BIASHARA

KWANINI MAFUTA YA KULA BEI JUU?

Huu hapa uhalisia wanaoibua mawaziri, vigogo wanaoshikilia kona zote kisekta

•Wizarani, viwadani, watafiti, madukani...

•Sababu ya shehena iliyoagizwa kupwaya

UKURASA 11


# Nipashe

Ijumaa Juni 4, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580601

www.ippmedia.com

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710


# MARUFUKU

**SERIKALI** yazuia biashara ya dawa asili ndani ya basi, faini mil. 10/-...*Endelea Uk. 2*



Wauza dawa za asili. **PICHA: MAKTABA**

## Kagame atuma ujumbe maalum kwa Rais Samia



UKURASA 2

## YALIYOMO


**UKURASA WA 2**

**KESI KUTEKWA KWA MO YAZUA JAMBO**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imesema hairidhishwi na mwenendo wa kesi ya Uhujumu Uchumi inayomkabili dereva taksi Mousa...

**UKURASA WA 4**

**SAKATA MAKINIKIA LAIBUKA BUNGENI**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amelieleza Bunge kuwa hakuna kontena la makinikia linalotoka nchini, kuuzwa pasipo serikali kupata mapato...


## SULUHISHO UHABA MAFUTA YA KULA

UKURASA 11

**MICHEZO** TAMASHA LA STARA KUFANYIKA JULAI UK. 23

MAONI, KATUNI UK. 6

# Kesi kutekwa kwa Mo yazua jambo

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imesema hairidhishwi na mwenendo wa kesi ya Uhujumu Uchumi inayomkabili dereva taksi Mousa Twaleb, anayedaiwa kushiriki kumteka Mohammed Dewji (MO), kutokana na kesi hiyo kutoendelea na mshtakiwa kusota gerezani mwaka wa tatu.

Hayo aliyabainisha jana Hakimu Mkazi Mkuu Huruma Shaidi, wakati kesi hiyo ilipotajwa huku Jamhuri ikiongozwa na Wakili Faraja Nguka, akidai upelelezi haujakamilika na washtakiwa wengine hawajakamatwa.

Hoja ya Nguka iliibua ubishani na Wakili wa utetezi, Mahfudhu Mbagwa, alidai shauri hilo ni la muda mrefu, Machi, mwaka huu upande wa Jamhuri ulidai kuna mtuhumiwa alikamatwa Afrika Kusini wanafanya utaratibu wa kumleta ili kumuunganisha katika kesi hiyo.

"Mheshimiwa Hakimu hawajasema kama wameshamleta au wamefikia wapi, wanasema kesi haiwezi kuendelea hadi washtakiwa wengine wakamatwe, naomba hatua zingine ziendelee kwa mshtakiwa aliyekuwa gerezani muda mrefu," alidai Wakili Mbagwa.

Akijibu Nguka alidai shauri ni la Uhujumu Uchumi, mwenye kuitolea uamuzi ni Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), ambaye tayari wameshaifikisha kesi hiyo kwake kwa sababu ni miongoni mwa kesi za muda mrefu.

"Kesi za muda mrefu tumeshafikisha kwa DPP, hii ikiwa moja wapo sababu yeye ndio mwenye kushtaki na kuachia," alidai Nguka.

Alidai mchakato wa kumleta mshtakiwa kutoka Afrika Kusini unaendelea, lazima nchi husika iridhie kwa sababu mtuhumiwa sio raia wa Tanzania ni raia wa Afrika Kusini.

Mshtakiwa aliomba kuzungumza na kudai hajawahi kumteka Mo na hata Mo mwenyewe hamjui.

Baada ya kumaliza kusikiliza hoja hizo, Hakimu Shaidi alisema shauri hilo ni la muda mrefu na mahakama hairidhishwi na mwenendo wa shauri hilo.

"Nimefikisha kesi hii mbele ya wahusika akiwemo mwakilishi wa DPP, mshtakiwa kama ana kosa aendelee kushtakiwa kwa kosa lake au apewe dhamana ya Polisi wakati akisubiri washtakiwa wengine wakamatwe.

"Nimelipendekeza hili shauri la muda mrefu na mwelekeo wake siuelewi," alisema Hakimu Shaidi na kuahirisha kesi hadi Juni 16, mwaka huu kwa ajili ya kutajwa.

Watuhumiwa wengine ambao upande wa mashtaka inawatafuta ni raia wanne wa Msumbiji na mmoja wa Afrika Kusini wanaodaiwa kumteka mfanyabiashara huyo.

Washtakiwa hao waliwataja kuwa ni Phila Tshabalala raia wa Afrika Kusini, Henrique Simbine, Daniel Manchice, Issac Tomo na Zacarious Junior wote raia wa Msumbiji.

Katika kesi hiyo inadaiwa Mei Mosi na Oktoba 10, 2018, katika maeneo ya jiji la Dar es Salaam na Johannesburg Afrika Kusini, kwa makusudi washtakiwa wote kwa pamoja waliendesha genge la uhalifu.

Pia inadaiwa Oktoba 11, 2018 maeneo Hoteli ya Colloseum, wilayani Kinondoni Dar es Salaam, Twaleb pamoja na watu wengine ambao hawapo mahakamani, walimteka nyara MO kwa nia ya kumuhifadhi kwa siri na kumuweka maeneo ambayo ni hatari.

Inadaiwa Julai 10, 2018 maeneo ya Mbezi Beach wilayani Kinondoni, Dar es Salaam, Twaleb alitakatisha Sh 8,000,000 wakati akijua fedha hizo ni zao la kosa la kushiriki genge la uhalifu.

MO alitekwa nyara Oktoba 11, mwaka 2018 alfajiri maeneo ya Hoteli ya Colloseum wakati akienda kufanya mazoezi na alipatikana Oktoba 20, mwaka huo huo katika eneo la Gymkhana.

# Marufuku kuuza dawa ndani ya mabasi

**Na Waandishi Wetu,** ARUSHA

WAFANYABIASHARA wa dawa na vipodozi vinavyotengenezwa na mimea ya asili ambao hutumia mabasi ya abiria kuziongezea sifa ambazo hazina katika kutibu magonjwa mbalimbali ya binadamu, wako mtegoni baada ya Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) kutangaza kiama dhidi yao.

Watakaonaswa kuanzia sasa katika operesheni maalum ya kudhibiti biashara hiyo, kama ni mtu binafsi, atatozwa faini ya Sh. 100,000 na kama ni taasisi, adhabu yake ni Sh. milioni moja hadi milioni 10.

Jana, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Dk. Yohana Mwalwisi, alisema kinachoendelea kufanywa na wafanyabiashara hao katika vyombo vya usafiri kwa sasa ni utapeli dhidi ya afya ya binadamu.

Akizungumza katika kikao kazi kati ya wahariri na waandishi wa habari wa mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro, Dk. Mwalwisi alisema:

"Ni kosa kisheria kuongeza uwezo wa dawa ili unufaike wakati hazina ubora huo. Kinachofanyika kwenye mabasi ni utapeli, kusifia dawa zao wanazokuwa wanauza na kuziongezea sifa ambazo hazina."

Kwa mujibu wa Kaimu Mkurugenzi huyo, watu wanaofanya matangazo hayo kwenye vyombo vya usafiri, wanahatarisha usalama na afya za watumiaji wa bidhaa hizo.

"Mfano hatujawahi kusikia hospitali au maabara zinatoa matangazo juu ya huduma wanazozitoa, hivyo wanaotoa matangazo hayo wanakosea," alionya.

Dk. Mwalwisi alisema sababu za wafanyabiashara hao kuendelea kutoa matangazo ni kutokana na uchache wa wafanyakazi wa TMDA, ambao hawawezi kuwa kwenye vyombo vya usafiri kwa wakati huo kudhibiti watu hao.

Alitumia fursa hiyo kuwaomba wananchi kutoa taarifa wanapoona watu wanatoa matangazo kwenye vyombo vya usafiri ili wachukulie hatua haraka iwezekanavyo.

Akifafanua zaidi kuhusu biashara hiyo, Mshauri wa Sheria wa TMDA, Iskari Fute, alisema watu waofanya matangazo ya aina hiyo, wanakiuka Sheria ya Udhibiti Dawa Na Vifaa Tiba, Sura ya 219.

Kutokana na katazo hilo la kisheria, Fute alisisitiza yeyote atakayekamatwa kwa kukiuka sheria hiyo kuanzia sasa, kama ni mtu binafsi atatozwa faini ya Sh. 100,000 na kama ni taasisi, adhabu yake inaanzia Sh. milioni moja hadi milioni 10.



Kaimu Mkurugenzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Dk. Yonah Hebron.

Vilevile, alisema TMDA inaziona faini hizo kama ni ndogo, hivyo ina mpango wa kupandisha tozo.

Mwongozo wa kimataifa wa tiba unazuia mtu au taasisi kutangaza biashara ya dawa na matibabu.

●**Imeandikwa na Jaliwason Jasson na Mary Mosha (Arusha)**

# Kagame amtumia ujumbe Samia



Rais Samia Suluhu Hassan akisoma ujumbe maalumu wa Rais wa Rwanda, Paul Kagame, baada ya kuwasilishwa kwake na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa wa Rwanda, Dk. Vincent Biruta, Ikulu ya Chamwino mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Paul Kagame wa Rwanda, amemhakikishia Rais Samia Suluhu Hassan, kuwa nchi yake ipo tayari kukuza zaidi uhusiano wake na Tanzania hususani katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Rais Kagame alituma ujumbe huo kwa Rais Samia uliowasilishwa na Mjumbe Maalum na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa wa Rwanda, Dk. Vincent Biruta.

Katika ujumbe huo, Rais Kagame ametuma salamu za pole kutokana na kifo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli, amempongeza Rais Samia kwa kupokea kijiti cha Urais na amemhakikishia kuwa Rwanda ipo tayari kukuza zaidi uhusiano na ushirikiano wake na Tanzania.

Taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Gerson Msigwa kwa vyombo vya habari jana, ilisema Kagame amesema hali ya Rwanda ni shwari, inaendelea kusukuma mbele maendeleo yake na ipo tayari kukuza zaidi uhusiano wake na Tanzania hususani katika utekelezaji wa miradi ukiwamo wa kuzalisha umeme wa Rusumo na ujenzi wa reli ya kisasa (standard gauge railway) ya kuunganisha Jiji la Kigali (Rwanda) na Isaka (Tanzania) ambayo itasaidia usafirishaji wa mizigo kutoka Bandari ya Dar es Salaam kwenda Rwanda.

Rais Samia amemshukuru Rais Kagame kwa kumtumia ujumbe huo uliojumuisha salamu za pole na pongezi na amemhakikishia kuwa Tanzania ipo tayari kukuza zaidi uhusiano na ushirikiano wake na Rwanda.

Kuhusu utekelezaji wa miradi ya pamoja, ametaka Tume ya Pamoja ya Ushirikiano wa Tanzania na Rwanda (JPC), ikutane ili kuongeza msukumo katika miradi hiyo pamoja na kuainisha maeneo mapya ya ushirikiano yenye maslahi kwa pande zote mbili.

Maeneo mengine ambayo ametaka JPC ifanyie kazi ni kuimarisha usafirishaji wa minofu ya samaki kutoka Mwanza kupitia Shirika la Ndege la Rwanda na kuharakisha ujenzi wa bandari kavu ya Isaka.

## HABARI KITAIFA



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Khamis Hamza Chilo, akimjulia hali mmoja wa majeruhi wa ajali ya basi la kampuni ya Classic linalofanya safari zake kati ya Uganda, Kampala na Dar es Salaam, lililopata ajali katika eneo la Buyubi, mkoani Shinyanga juzi, katika Hospitali ya mkoa huo jana. **PICHA: WMNN**

# Taasisi za kiraia zasisitiza usafi kazini

**Na Maulid Mmbaga**

TAASISI ya kiraia ya Shahidi wa Maji inashirikiana na kampeni ya taifa ya usafi wa mazingira 'Nyumba ni choo' kufanya uhamasishaji wa wafanyakazi kuzingatia kanuni za usafi katika maeneo ya kazi ili kujiepusha na magonjwa ya mlipuko.

Hayo yalisemwa jana na balozi wa kampeni hiyo, Elias Barnaba, wakati walipotembelea kiwanda cha Tooku kinacho jihusisha na ushonaji wa nguo, Ubungo jijini Dar es Salaam, kwa dhumuni la kuhamasisha wafanyakazi kuchukua tahadhari za kiafya dhidi ya mlipuko wa magonjwa.

Alisema kampeni hiyo ya uhamasishaji inayoendeshwa kwa kaulimbiu ya 'Siri ya Usafi ni Kubalance' ilitanguliwa na utafiti uliofanyika viwandani na maeneo ya karibu ili kubaini kiwango cha uzingatiaji wa kanuni za usafi miongoni mwa wafanyakazi.

Pia alisema utafiti huo umeonyesha kwamba uzingatiaji wa kanuni za usafi kama kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni, kuzingatia umbali kati ya mtu na mtu na usafi wa uso ni muhimu zaidi viwandani kuliko nyumbani au maeneo mengine.

"Tunaposema siri ya ushindi ni kubalansi tunalenga kuhamasisha wananchi kuendelea kuzingatia kanuni za usafi wanapoendelea na kazi zao za kila siku. Sisi Tanzania ni kati ya mataifa machache sana duniani ambao tuliendelea na shughuli zetu baada ya mlipuko wa ugonjwa wa corona.

"Hata hivyo, tulikuwa tukifanya kazi huku tukizingatia tahadhari za usafi na hii ndiyo siri ya ushindi wetu ambayo hatutakiwi kuusahau," alisema Barnaba.

Kampeni hiyo ni mwendelezo wa jitihada za serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuhamasisha wananchi kuendeleza tabia ya kuzingatia kanuni za usafi ili kuwa salama wakati wote.

"Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akisisitiza Watanzania wote kuendelea kuzingatia kanuni za usafi ili kujikinga na magonjwa ya mlipuko," alisema Barnaba.

Meneja Usimamizi wa kampuni ya Tooku, Franziska Jautz, aliishukuru kampeni hiyo na kusema itaongeza hamasa ya wafanyakazi kuzingatia kanuni za usafi hata wakiwa kwenye maeneo yao ya nyumbani.

"Hapa tuna wafanyakazi zaidi ya 3,700 kwahiyo usalama na afya ya kila mmoja ni muhimu sana," alisema Franziska.

# Mbaroni tuhuma kumuua mpenzi

**Na Francis Godwin,** IRINGA

JESHI la Polisi Mkoa wa Iringa, linamshikilia mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Iringa, Prudence Patrick (22) kwa tuhuma za kumuua kwa kumnyonga shingo mpenzi wake Petronila Mwanisawa (21), mkazi wa Semtema, Kata ya Kihesa, Iringa.

Imedaiwa kuwa mtuhumiwa wa mauaji hayo ni mwenyeji wa Sumbawanga na ni mwanafunzi wa kozi ya uandishi wa habari na marehemu pia alikuwa mwanafunzi mwenzake na alikuwa mwenyeji wa Mkoa wa Kagera.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Iringa, Juma Bwire, aliwaambia waandishi wa habari jana ofisini kwake kuwa tukio hilo lilitokea majira ya 12 alfajiri katika eneo la Semtema, Kata ya Kihesa, Manispaa ya Iringa kwenye chumba alichokuwa akiishi mtuhumiwa huyo.

Alisema kuwa mwanafunzi anayedaiwa kunyongwa, alifika nyumbani kwa mtuhumiwa huyo usiku wa kuamkia Juni Mosi mwaka huu akiwa na rafiki yake aliyefahamika kwa jina la Belnada Njafula kwa lengo la kuchukua pesa yake kiasi cha Sh. 5,000 ambayo alikuwa anamdai mpenzi wake huyo.

"Baada ya kufika nyumbani kwa mtuhumiwa rafiki yake aliondoka na kuwaacha wawili hao kwa muda ili walipane deni walilokuwa wakidaiana.

"Hata hivyo, marehemu hakurudi nyumbani kwao hadi pale mwili wake ulipokutwa ndani ya chumba cha mtuhumiwa ukiwa umefungiwa ndani na umelazwa kitandani ukitokwa na povu mdomoni na damu puani," alisema Kamanda Bwire.

Alidai kuwa taarifa za awali za kiuchunguzi zinaonyesha mtuhumiwa baada ya kufanya unyama huo, alitumia simu ya marehemu kutumiana ujumbe na rafiki yake kumjulisha kama ana mimba ya Jay ambaye ni rafiki yake.

"Mtuhumiwa alitumia simu ya marehemu kuchati na rafiki wa marehemu kumjulisha kuwa ana mimba ya Jay na baadaye kuwajulisha wazazi wa marehemu kuwa 'binti yenu amefariki dunia'," alisema.

Kamanda Bwire alisema taarifa za awali kuhusu kifo cha mwanafunzi huyo zilitolewa na wazazi wake kutokana na taarifa walizotumiwa na kijana huyo mtuhumiwa.

Alisema kuwa baada ya kufanya unyama huo, mtuhumiwa alikamatwa na Jeshi la Polisi akijaribu kutoroka kuelekea mkoani Dodoma na alikamatwa maeneo ya Mgongo kilomita chache kutoka maeneo ya Semtema anakodaiwa kufanya mauaji hayo.

Kamanda Bwire alisema mtuhumiwa anashikiliwa na polisi na upelelezi wa tukio hilo unaendelea na pindi utakapokamilika, atafikishwa mahakamani.



# Sakata makinikia laibuka bungeni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amelieleza Bunge kuwa hakuna kontena la makinikia linalotoka nchini, kuuzwa pasipo serikali kupata mapato stahiki.

Aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Msalala (CCM), Iddi Kassim Iddi, ambaye alisema serikali ilizuia usafirishaji wa makinikia nje ya nchi lakini kwa sasa Watanzania wameshuhudia makontena hayo yakisafirishwa kupitia barabara ya Bulyankulu -Kahama na Bandari ya Dar es Salaam.

Akijibu swali hilo, Waziri Mkuu Majaliwa alisema: "Makontena yote yanayosafirishwa tayari yameshauzwa na serikali imeshapata fedha yake, fedha imeshahifadhiwa kwenye akaunti zetu kwa hiyo Watanzania hatupati hasara na hatua inayofuata mnunuzi anakuwa huru kuyapeleka anapotaka."

"Ndiyo hayo makontena yanayoonekana kutoka, kwa hiyo Watanzania kuyaona makontena yakipita niwatoe hofu kuwa makontena hayo yameshauzwa tayari na huyo ni mnunuzi,"alisema Majaliwa.

Aidha, Waziri Mkuu aliwaomba Watanzania kuondoa mashaka juu ya usafirishaji wa makontena hayo yenye makinikia kwa sababu serikali inayo timu kwenye mgodi kuhakiki ya kuhakikisha fedha inalipwa.

"Lakini hakuna kontena la makinikia linalotoka nchini bila kuuzwa, lakini tumeweka timu pale bandarini kuhakikisha kila kontena la makinikia linaloingia pale lina nyaraka zote baada ya kufanya mauzo huko huko kwenye mgodi, kwa hiyo hakuna kontena linaibiwa,"alisema Majaliwa.

Alisema serikali ipo makini na wataalamu wa maeneo hayo waendelee kuwa makini kuhakiki nyaraka za kuuza makinikia hayo.

"Tunaingiza fedha za kutosha sina takwimu kwasasa lakini tunaingiza fedha za kutosha, Waziri wa Madini alipokuwa akiwasilisha bajeti yake alitoa ufafanuzi na kuonesha namna sekta ya madini ilivyopata kiasi kikubwa sana,"alisema na kuongeza:

"Nataka niwakumbushe Watanzania kwenye hili kwamba serikali mwaka 2017/18 tulizuia usafirishaji wa makinikia kwenda nje ya nchi kwasababu yalikuwa hayajafuate utaratibu, lakini pia kulikuwa na udanganyifu mkubwa na tulipozuia makontena zaidi ya 300-400 bandarini yalikaa pale mpaka tulipoweka utaratibu". Alisema Majaliwa.

Aliongeza:"Utaratibu uliowekwa na serikali kwanza kuwatambua ni nani anasafirisha makinikia kwenda nje na nani wametoa vibali hivyo kwenda nje na tukazuia kabisa tukaanza utaratibu mpya."

Waziri Mkuu Majaliwa alisema: "Rais Hayati John Magufuli alisimamia na kwa kuunda timu iliyofanya uhakiki wa sekta yote ya madini ikiwamo eneo la usafirishaji wa mchanga ambalo tulikuwa tunaibiwa kwa kiasi kikubwa." "Ufumbuzi wa ile timu ni kuanzisha kampuni ya Watanzania kwa ushirikiano na kampuni za nje yaliyopo hapa nchini na leo hii tunayo kampuni inaitwa Twiga ambayo ni ya serikali ambayo imeingia ubia na wachimbaji wakubwa wa madini ambapo migodi mikubwa chini ya Barrick tumetengeneza kampuni moja,"alisema.

Alifafanua kuwa kwanza wataalamu wanapitia kujua aina zote za madini na mwanzo waliambiwa kuna madini ya aina moja tu ya dhahabu lakini baada ya uchambuzi wa wataalamu wamegundua aina tano.

"Kwa hiyo leo hii kupitia kampuni yetu ya serikali inauza madini aina zote tano, tukishagundua udongo na aina zote tunayauza hapa hapa ndani ya nchi na siyo nje ya nchi,"alisema Majaliwa.

Katika hatua nyingine, Mbunge wa Dodoma mjini (CCM), Anthony Mavunde, alihoji mkakati wa serikali katika kuhakikisha takwa la kisheria la taasisi nunuzi kutenga asilimia 30 ya zabuni yake kwa ajili ya vikundi vya akina mama, vijana na watu wenye ulemavu.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi akizungumza na Mwakilishi Mkaazi wa UN Women nchini Tanzania, Hodan Addou, alipofika Ikulu jijini Zanzibar jana, kwaajili mazungumzo na kujitambulisha. **PICHA: IKULU**

# Hatima ya Seth mikononi mwa DPP

**Na Kulwa Mzee**

KESI ya uhujumu uchumi inayomkabili Mkurugenzi wa Kampuni ya Kufua Umeme (IPTL), Herbinder Seth, inasubiri mwongozo wa Mkurugenzi mpya wa Mashtaka (DPP) ili kumaliza mazungumzo ya kumaliza kesi hiyo.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi, wakati kesi hiyo ilipokuja kwa ajili ya kutajwa na kujua hatua iliyofikia katika mazungumzo hayo.

Kesi hiyo iliyokuja kwa ajili ya kutajwa, upelelezi wake haujakamilika na mazungumzo yaliyokuwa yakifanyika kwa ajili ya kumaliza kesi dhidi ya mshtakiwa Seth yanaendelea pale yalipoishia, yakisubiri mwongozo kutoka kwa DPP mpya aliyeteuliwa hivi karibuni na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan.

Mshtakiwa Seth na Wakili Joseph Makandege, waliwasilisha ombi kwa DPP wakionesha nia yao ya kutaka kumaliza kesi kwa kukiri makosa yao lakini, Mei 6, mwaka huu, Wakili Makandege, aliondoa nia yake ya kufanya mazungumzo na DPP akieleza kwamba mazungumzo hayo hayana afya na yamechukua muda mrefu kukamilika.

Mbali na Seth washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni mfanyabiashara James Rugemalira na wakili Makandege

Rugemarila, ambaye ni Mkurugenzi wa VIP na mmiliki mwenza wa zamani wa IPTL na Seth ambaye ni Mwenyekiti Mtendaji wa PAP, wanadaiwa kutenda makosa hayo katika Jiji la Dar es Salaam na nchi za Afrika Kusini, Kenya na India.

Washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka 12 yakiwamo ya utakatishaji fedha, miongoni mwa mashtaka hayo yapo ya kula njama, kujihusisha mtandao wa uhalifu, kughushi na kutoa nyaraka za kughushi na kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu, kutakatisha fedha na kusababisha hasara ya Dola za Marekani 22,198,544.60 na Sh. 309,461,300,158.27.

Wanadaiwa kati ya Oktoba 18, mwaka 2011 na Machi 19, mwaka 2014 jijini Dar es Salaam walikula njama katika nchi za Afrika Kusini, Kenya na India ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Mwanasheria Makandege, anakabiliwa na mashtaka matano likiwamo la kuisababishia serikali hasara ya Dola za Marekani 980,000.

# NEC yapuliza kipenga uchagzuzi mdogo Z'bar

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imepuliza kipenga cha uchaguzi mdogo wa ubunge katika Jimbo la Konde, Wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba, pamoja na kata sita za Tanzania Bara ambao utafanyika Julai 18, mwaka huu.

Uchaguzi unafanyika baada ya kutokea kwa kifo cha aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo, Khatibu Said Haji.

Akitoa taarifa ya uchaguzi huo, Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Dk. Wilson Mahera, alisema tayari NEC imepokea barua kutoka kwa Spika wa Bunge kuwa kiti hicho kiko wazi.

"Tume ilipokea barua kutoka kwa Spika wa Bunge, ambaye kwa kuzingatia kifungu cha 37 (3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, ameitaarifu tume uwapo wa nafasi ya wazi ya kiti cha ubunge katika Jimbo la Konde, Wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba," alisema Dk. Mahera.

Alisema NEC imepokea barua kutoka kwa waziri mwenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) akiitaarifu juu ya kuwapo kwa nafasi wazi za madiwani kwenye kata sita za Tanzania Bara.

"Kwa kuzingatia masharti ya Kifungu cha 37(1)(b) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Kifungu cha 13 (2) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume imeandaa chaguzi ndogo ili kujaza nafasi ya mbunge iliyowazi katika Jimbo la Konde na nafasi za udiwani kwenye kata sita za Tanzania Bara," alisema Dk.Mahera.

Alizitaja kata zitakazohusika katika uchaguzi huo ni Kata ya Mbagala Kuu Manispaa ya Temeke mkoani Dar es Salaam, Kata ya Diringish iliyopo Kiteto, Wilaya ya Kiteto mkoani Manyara, Kata ya Mitesa, Lulindi, Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara.

Zinine ni Kata ya Gare, Lushoto Wilaya ya Lushoto mkoani Tanga, Kata ya Mchemo, Newala Vijijini, Wilaya ya Newala mkoani Mtwara na Kata ya Chona, Ushetu, Wilaya ya Ushetu mkoani Shinyanga.

Alisema maandalizi kwa ajili ya uchaguzi huo yameshafanyika na kazi ya utoaji fomu za uchaguzi kwa wagombea inaanza Juni 21 hadi 27,2021 huku uteuzi wa wagombea watakaowania nafasi hizo ukifanyika Juni 27 mwaka huu.

Aidha, Dk. Mahera alisema kampeni za uchaguzi Konde na kata utaanza Juni 28, 2021 na zitafikia ukomo Julai 17 mwaka huu na uchaguzi kufanyika 18 Julai,2021.

Alisema tayari NEC imevitaarifu vyama vya siasa kwa njia ya barua juu ya kuwapo kwa uchaguzi huo mdogo na inavikumbusha kuzingatia sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi, miongozo na maelekezo ya tume wakati wote wa kipindi cha uchaguzi.

HABARI KITAIFA

# Mwinyi: Hiki ndicho kiini kubinafsisha mashirika

**Na Christina Mwakangale**

RAIS mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi (pichani) ametaja sababu zilizoisikuma serikali kubinafsisha mashirika ya umma.

Katika kitabu chake cha 'Mzee Rukhsa, Safari ya Maisha Yangu', Mwinyi anasema moja ya sababu hizo ni kitendo cha mashirika hayo kugeuka waomba msaada badala ya kutoa msaada.

Anasema kutokana na matatizo katika mashirika hayo hasa uzembe, rushwa na ubadhirifu pamoja na uwezo mdogo wa menejimenti, uongozi, uzoefu duni wa kuzilinda mali zilizokabidhiwa, aliamua kufanya mageuzi ili kuulinda uchumi kwa kuyabinafsisha.

Anasema uendeshaji mbovu hadi kubinafsishwa mashirika ya umma ni moja ya mambo yanayouma hadi sasa.

"Baada ya Azimio la Arusha, tulitaifisha kampuni, biashara na huduma binafsi, zikiwamo shule na huduma za afya, serikali ikiwekeza zaidi kwenye kuanzisha mashirika mapya ya umma.

"Mwalimu, na sisi sote tuliamini kuwa mashirika haya yatazalisha faida kubwa. Maana tangu hapo walikuwa na ukiritimba wa bidhaa na biashara," anasimulia.

Mwinyi anasema kilichotokea kwenye mashirika hayo ni utekelezaji duni, ambao haukuleta matumini na mafanikio kutokana na ushahidi uliokuwapo kinadharia.

"Ulikuwapo ushahidi wa kutosha kuwa utekelezaji wake, haukuleta matumaini ya mafanikio na badala yake mashirika mengi ya umma yakawa yanaomba msaada badala ya wao kuwa msaada.

"Mashirika yalijiingiza kwenye gharama zisizohusika na kazi zao za msingi na kuchangia kuongeza hasara. Mfano, mashirika yaliajiri wafanyakazi wengi kuliko mahitaji halisi.

"Ilikuwa kama mashindano, kila shirika kuwa na hospitali yake, idara yake, usafiri, vikundi ya michezo na utamaduni," anabainisha.

Mwinyi anaitaja hasara iliyopata mashirika hayo baada ya ripoti ya Shirika la Ukaguzi la Tanzania 1992/93, kusema miongoni mwa mashirika 345 yaliyokaguliwa, machache yalipata faida ya Sh. bilioni 51.2 kabla ya kodi; huku mengi yakipata hasara ya jumla ya Sh. bilioni 97.2 na kuchangia kukua kwa deni la taifa.

"Kwa maneno mengine, kwa ujumla wao waliitia serikali hasara ya Sh. bilioni 46 kwa mwaka mmoja tu.

"Kwa thamani ya fedha ya wakati huo. Ilifika mahali wapenda mzaha wakakibatiza kifupi cha Shirika la Umma 'SU' kuwa 'Sina Uchungu'. Hiyo ndiyo hali halisi ya mashirika ya umma mengi niliyoikuta nilipoingia madarakani," anasimulia.

Mwinyi anasema kati mambo ambayo yanahusishwa na utawala wake, mojawapo ni mageuzi makubwa kiuchumi na kulazimika kujitwisha mzigo, akisisitiza kwa tafsiri yake kwamba 'Lisilo Budi Hutendwa; Mageuzi ya Uchumi Yalikuwa Lazima'.



# Mbunge adai kutishiwa kifo

**Na Romana Mallya**

MBUNGE wa Sengerema, Hamis Tabasamu (CCM), amesema ametishiwa maisha baada ya kupeleka bungeni taarifa ya uwekaji vinasaba na kumwomba Spika wa Bunge, Job Ndugai, kumpa ulinzi.

Akichangia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2021/22, Tabasamu alisema juzi bungeni kuwa kampuni iliyokuwa imepewa zabuni hiyo, kila mwezi huchukua Sh. bilioni tano na kwa mwaka ni Sh. bilioni 60 ambayo ni bajeti ya karibu wizara tatu.

"Huyu mtu amechukua Sh. bilioni 60 hadi Sh. bilioni 70 kwa miaka sita ambapo ni karibu Sh. bilioni 450 halafu wabunge tunakuja kuzungumzia kampuni ya vinasaba, sasa hivi badala ya kujipa pole kwa kazi hii, vinasaba ni nini?

Vinasaba ni mafuta haya haya, petroli hii hii kinachowekwa ni kemikali tu.

Alisema mkataba wake uliisha Septemba mwaka jana akaongezewa.

"Mwezi wa Desemba mkataba umeisha akaongezewa miezi mitatu, Februari 28 mwaka huu kaongezewa miezi mitatu, inaumiza sana katika roho," alisema.

Tabasamu alisema wakati wanasema TBS ifanye kazi hiyo wengine wanasema suala halina sheria.

"Tunaomba tafsiri ya neno TBS ni nini? Hili ni shirika la viwango la taifa, viwango vya aina yoyote iwe gesi, mafuta, dawa, sheria gani ije iundwe kwa ajili ya TBS?" alihoji.

Tabasamu alisema kwa sababu vinasaba vinatengenezwa maabara, TBS akiwezeshwa wafanyakazi, miundombinu na kununua mashine na kuwatengeneza wataalamu, inaweza kufanya kazi hiyo kwa sababu ni suala la usalama wa nchi na halitakiwi kuachiwa mtu.

Wakati Tabasamu akiendelea na mchango wake, Mbunge Gairo, Ahmed Shabiby, alimwomba Spika Ndugai taarifa na kueleza kuwa TBS ikifanya kazi hiyo, fedha zitaingia kwenye mfuko wa serikali kuliko inavyofanywa na mtu binafsi.

Mbunge huyo aliliambia Bunge kuwa ametishiwa maisha kutokana na suala hilo baada ya kupeleka habari zake bungeni.

"Nilimwambia Spika na kesi hii ipo kwa Kamanda wa Polisi Dodoma, na hatujapata majibu ya walionipigia simu na namba zao zipo pale kwa ajili ya kunitisha na kujua kazi hiyo imefanyika wapi?

"Mheshimiwa Spika na hili unisaidie kunilinda kwa ajili ya uzalendo, nimeleta jambo hili kwa sababu tunataka fedha za barabara za TARURA (Wakala wa Barabara Vijijini)," alisema.

Spika Ndugai alisema ipo haja ya kupelekewa bungeni sheria ambayo itaiwezesha TBS kufanya kazi hiyo kwa misingi ya kisheria bila kuingiliwa na mtu yeyote.



## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Madereva wadhibitiwe kupunguza ajali

**KATIKA** toleo letu la jana la gazeti tuliripoti tukio la ajali ya basi iliyotokea wilayani Shinyanga ikihusisha basi la Kampuni ya Classic na kusababisha vifo vya watu wanne.

Ajali hiyo pia ilisababisha majeruhi 20 huku wengine wakikatika viungo vya mwili.

Inasikitisha kuona kila mwaka matukio ya ajali barabarani yakiendelea kupoteza maisha ya Watanzania kutokana na uzembe wa madereva ambao wengi wao hawafuati sheria za barabarani.

Katika ajali hiyo, abiria walieleza kuwa basi walilokuwamo lilikuwa katika mwendo kasi hali iliyosababisha dereva kushindwa kulimudu gari alipofika kwenye kona.

Udhibiti wa mwendokasi barabarani ni moja ya hatua ambazo zimekuwa zikichukuliwa na Kikosi cha Usalama Barabarani cha Jeshi la Polisi kila wakati, lakini cha kushangaza madereva bado hawachukui tahadhari.

Jitihada hizo licha ya kuwa na nia njema ya kuhakikisha matukio ya ajali yanapungua kama siyo kumalizwa kabisa, zimekuwa kiziwachukiza baadhi ya abiria ambao wamekuwa wakilalamikia udhibiti huo unao wachalewesha kufika mapema.

Siyo abiria tu hata madereva nao wanajali zaidi kufika mapema maeneo wanayokwenda badala ya kujali usalama wa maisha yao na ya wengine.

Miongoni mwa hatua zilizosababisha udhibiti wa mwendokasi na ajali kupungua ni faini na matumizi ya tochi za trafiki.

Kadhalika, kupanga muda wa kuondoka na kufika kwa mabasi ya mikoani kumechangia kwa kiwango kikubwa kudhibiti ajali za barabarani, lakini baadhi ya askari wa usalama wamekuwa wakipokea rushwa ya kuyaruhusu magari ambayo yamefika kituo X kabla ya muda uliyopangiwa.

Ni wakati mafaka sasa kwa Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani kuendelea kuchukua hatua kali za udhibiti wa mwendokasi pasipo kumuonea haya dereva yeyote.

Kukithiri kwa ajali za barabarani nchini hata kusababisha watu wengi kupoteza maisha, kunaleta hofu kubwa hususani kwa watumiaji wa usafiri wa barabara wa kutokuwa na uhakika wa usalama wa maisha yao.

Hali ya Watanzania wengi kimapato ni duni, hawawezi kutumia usafiri wa anga, wengi wao wanatumia wa barabara kwa kupanda mabasi, lakini hofu ya ajali za kizembe zitawalazimisha Watanzania kuogopa kusafiri.

Pamoja na juhudi zinazofanywa na Kikosi cha Usalama Barabarani katika kuhakikisha kuwa, kanuni na sheria za usalama barabarani zinazingatiwa ili kuleta utatuzi wa hilo, mwenye jukumu kubwa la kuhakikisha ajali za kizembe hazitokei ni dereva pamoja na abiria waliopanda chombo hicho.

Kwa namna yoyote ile, juhudi zaidi zinahitajika ili kubaini kiini au chanzo cha ajali ambazo kila mwaka 'zinameza' Watanzania, na kuacha simanzi kwa familia nyingi kufiwa na wapendwa wao, kusababisha majeruhi, ulemavu wa kudumu na upotevu wa mali.

Kuna kila sababu ya kuchukua hatua za haraka ili kupunguza na kudhibiti ajali hizi kwa lengo la kuokoa maisha ya watu na mali zao.

Hayati Rais John Magufuli, alikaririwa akiwakumbusha watumiaji wa barabara hasa madereva kuwa makini na kuzingatia sheria za usalama barabarani.

Tunakubaliana na kuunga mkono hatua kadhaa za udhibiti wa mwendokasi barabarani na tunaona itakuwa vizuri na muhimu zaidi ikiwa sheria ya usalama barabarani itafanyiwa maboresho kwa lengo la kuyadhibiti zaidi magari ya abiria.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Bajeti Kuu hiyo njiani kusomwa, nasi wadau tuna haya juu yake

Na Yasmine Protace

**BAJETI** Kuu ya serikali inatarajiwa kusomwa Juni 10, mwaka huu. Hivyo, tunategemea kuona mafanikio makubwa yakitekelezwa kupitia bajeti hiyo, kugusa moja kwa moja maslahi yao.

Hiyo ni kutokana na kupitishwa makadirio ya mapato na matumizi ya kila wizara, Watanzania wanatarajia kuona neema inapatikana kupitia vipaumbele vikitakavyotajwa kwao.

Baadhi ya washiriki wa semina za Jinsia na Maendeleo (GDSS), zinazoratibiwa na asasi TGNP Mtandao, wanazungumzia maoni yao katika Bajeti Kuu ya Serikali kwa Mwaka 2021/22, kwa matarajio na jicho la kipekee katika sekta za maji, elimu, afya na kilimo.

Nyajura Kalingo, anasema matarajio yake katika sekta ya maji ni upatikanaji huduma hadi vijijini, akigusa magumu yaliyoko kupitia baadhi ya miundombinu kuharibika na kusababisha upotevu wa maji.

Anasema, kuwapo wataalamu watakaojikita katika ufuatiliaji maji na wanapogundua kuna changamoto, wazitatue huku akitamka haja ya kuwapo miradi mikubwa itakayosaidia kupunguza uhaba wake.

"Kuwapo na maboresho ya mabomba ili kuhakikisha maji hayapotei," anasisitiza namna kunavyokuwapo miundombinu ya kiteknolojia, itasaidia maji yasipotee.

Mwajuma Idrisa, anasema katika sekta ya elimu matarajio yake ni miundombinu yake iboreshwe, matundu ya vyoo yaongezeke, kulingana na idadi ya wanafunzi shuleni.

"Tuneona kuna changamoto katika matundu ya vyoo katika baadhi ya shule, ambako wanafunzi ni wengi lakini matundu ya vyoo ni machache," anasema.

Maoni yake kuhusu bajeti kuu ni kwamba, shule zinapaswa kuwa na matundu ya vyoo vya kutosha na kufanya hivyo kutasaidia hata watoto wa kike kuweza kujistiri vyema wanapokuwa katika hedhi.

Anataka kuwapo usawa wa kijinsia katika elimu, kwa sababu zipo shule ambazo ni za ufundi zimewalenga wanaume tu kusoma.

Katika afya, Kelvin Mlongo, anasema matarajio yake ni kuona inafutwa tozo kwa wajawazito na rai yake ni bajeti iruhusu tozo kwa wajawazito iondolewe.

Hapo ni katika vifaa vya kujifungua viwe bure na anasema mtu anapoumwa, akalazwa na kulipa bili sawa, lakini mtu anapokufa asidaiwe pesa.

"Umeuguza mgonjwa, umelipia kila kitu, huyo mgonjwa anapofariki maiti inatakiwa isitolewe mpaka ilipiwe, sasa kufanya hivyo inaleta usumbufu, tunaomba bajeti ya afya itoe kipengele cha maiti kudaiwa," anasema. Kelvin anaweka matarajio yake katika bima ya afya, itakuwa na maboresho, ili zinapotolewa ziwe na uwezo wa kuhudumia matibabu yote na sio kuchagua kadhaa.

Hoja inasonga pia kwa matibabu ya wazee yanapaswa kutolewa bure, kutokana na ukweli baadhi yao wanakosa uwezo wa kijitibu, vivyo hivyo huduma za afya zisogezwe karibu waliko wananchi, ili zahanati ziwe za tembezi 'mtaa kwa mtaa.'

Ni ufafanuzi unaosonga mbali, kutahadharisha kama mtu atakuwa na tatizo, asendelee kupatiwa matibabu, pia kuwapo vizimba vya kuchoma taka ngumu katika vituo vya afya na zahanati.

Maoni mengine aliyonayo, ni kuitaka serikali iwasaidie wahitaji wasio na uwezo, wanaotaka kusoma masuala ya afya, wafikiriwe.

Katika suala la kilimo, nimependa la Neema Mwinyi, kwamba serikali inapaswa kutoa elimu ya kilimo cha kisasa, jambo ninaloamini litamwezesha mkulima kunufaika na kilimo chake kipatiwe pembejeo kwa wakati.

Maoni ya nyongeza, ni serikali iwasaidie wakulima kwa kuwapa bei elekezi, maana wengi hawajui watauza wapi bidhaa zao.

Inapendeza kuona pale maofisa ugani wanapojenga utaratibu kutembelea wakulima ili waione majukumu yao.

Mzizi mwingine, ni haja ya vyama vya ushirika vitavyokuwa mkombozi kwa wakulima, kutokana na madalali waliopo wanachangia kuwadidimiza wakulima. Rai kuu,bajeti itengwe kwa wakulima na iwe na mwongozo kijinsia kuwanufaisha kinamama.

Kutoka kwake dada Aziza Akida, anagusia wanawake wanaathirika sana kiafya, hivyo kunatakiwa utaalamu wa ziada kuwadudumia, pia vitendea kazi.

Anasogeza haja ya kuwekeza mitaji mikubwa na kuboreshwa biashara za madini, huku takwimu ziwe katika mlengo wa kijinsia.

Ni mtazamo unaobeba maoni ya haja ya fidia kwa wananchi, pale wanapochukuwa ardhi yenye madini, ili kusiwapo migogoro na wizara zishirikiane na wataalamu kuwaibua wananchi.

# Jafo aagiza maofisa kusimamia sheria

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imewataka Maofisa Mazingira nchini kusimamia Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 kwenye maeneo yao ili kutekeleza kampeni ya kudumu ya usafi na utunzaji wa mazingira.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua semina ya maofisa hao, jijini hapa.

Alisema suala la utunzaji wa mazingira ni ajenda muhimu ambayo maofisa hao wanapaswa kuisimamia.

Alisema Sheria ya Mazingira imeelekeza jinsi gani wanajenga mazingira kwa kusimamia Sheria, Sera na Kanuni zake ili mazingira yalindwe.

"Maofisa mazingira mna kazi kubwa ya kufanya kuhakikisha Sheria ya Mazingira inasimamiwa, kampeni inayoenda kuzinduliwa nyinyi ndio mtakuwa wasimamizi wakuu, nataka maofisa mazingira sasa mfanyekazi," alisema.

Alisema ajenda ya mazingira ni muhimu na dunia inataabika na uharibifu wa mazingira ikiwamo uharibifu wa misitu ya asili na ya kupanda ambayo inachomwa moto na kusababisha hali ya mazingira kuwa mbaya katika maeneo mbalimbali.

Kutokana na uharibifu huo, alisema ndio maana kina cha maji ya bahari kimeongezeka na kila mwaka hekari milioni 48 zinapotea.

"Katika mitaa yetu tunayoishi tujitathimini suala la uchafu, maofisa mazingira mmepewa jukumu la kusimamia, tukiangalia katika mitaa yetu suala la usafi haliridhishi madampo yanapowekwa maeneo mengine hayatumiki vizuri, miundombinu ya majitaka haipo rafiki, usafi wa mifereji maeneo mengine hauridhishi, lakini ajenda ya nyumba na familia moja moja katika uimarishaji wa mazingira katika maeneo ya makazi nayo haipo vizuri," alisema.

"Tumekuwa na utaratibu wa kila mwaka kupanda miti, lakini hatuitunzi, tunajisifu tumepanda miti milioni moja nenda mwaka unaofuata hesabu miti inayoendelea kukua inawezekana hata mia moja haifiki, hivyo katika ajenda ya mazingira tuna jambo kubwa la kufanya," alisema.

Kwa upande wake, Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, alitoa maelekezo kwa Mamlaka za mitaa na sekretarieti za mikoa kuifanya ajenda ya utunzaji wa mazingira inakuwa ni ya kila siku.

Aliongeza kuwa kila mkoa na Mamlaka za Serikali za mitaa zihakikishe shule, vyuo, hospitali na vituo vya afya vilivyopo katika maeneo yao vinatumia nishati mbadala.

Awali, Katibu Mkuu wa ofisi hiyo, Mary Maganga, alisema semina hiyo ina lengo la kujadili na kutoa mapendekezo katika matatizo mbalimbali wanayokabiliana nayo katika maeneo yao.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Dk. Maduhu Kazi, akizungumza na wadau wa mbolea jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kuhusu ujenzi wa kiwanda cha mbolea kinachotarajiwa kujengwa na mwekezaji Aliko Dangote. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Usajili Vicoba waongezwa miezi sita

**Na Salome Kitomari**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imeongeza muda wa miezi sita kwa usajili wa vikundi kwa mujibu wa sheria ya huduma ndogo za fedha.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Gavana wa BoT, muda wa usajili umeongezwa hadi Novemba 30, mwaka huu.

"Kutokana na changamoto zilizojitokeza katika usajili wa vikundi vya kijamii vya huduma ndogo za fedha, Waziri wa Fedha na Mipango ameridhia kuongeza muda wa miezi sita zaidi kwa ajili ya usajili wa vikundi hivi," ilisema taarifa hiyo.

Taarifa hiyo ilisema muda huo wa ziada hauhusu watoa huduma ndogo za fedha wa daraja la pili, benki ndogo, kampuni za watu binafsi wala la tatu vyama vya ushirika.

Ilisema muda huo umeongezwa kutokana na changamoto za TEHAMA zilizojitokeza wakati wa usajili, na vikoba vingi kushindwa kukamilisha usajili.

Mwezi Desemba 2019, BoT ilitoa taarifa kwa umma kuhusu sheria ya huduma ndogo za fedha ya mwaka 2018 iliyoanza kutumika rasmi Novemba mosi, mwaka 2019.

Pamoja na mambo mengine, taarifa hiyo ilirejea kifungu cha 57 cha sheria ambacho kinawataka watoa huduma ndogo za fedha wote kuwasilisha maombi ya leseni au usajili BoT au kwenye mamlaka kasimishwa katika kipindi cha miezi 12 baada ya sheria kuanza kutumika, Oktoba 31, 2020.

Muda huo uliongezwa kwa miezi sita hadi 30 Aprili 2021 ili kuwapa watoa huduma ndogo za fedha katika madaraja yote muda wa ziada wa kuandaa na kuwasilisha maombi ya usajili na leseni kwa mamlaka za usajili na usimamizi.

# TIC kumpa Dangote eneo la kiwanda

**Na Mwandishi Wetu**

KITUO cha Uwekezaji Nchini (TIC), kimesema kimepata ardhi ya kutosha kwa ajili ya kumpatia mfanyabiashara mashuhuri Afrika, Alhaji Aliko Dangote, ambaye ameahidi kujenga kiwanda kikubwa cha kuzalisha mbolea.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa Kituo hicho, Dk. Maduhu Kazi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu hatua ambazo kituo hicho kimechukua kumsaidia mwekezaji huyo.

Dangote ambaye amewekeza kwa kiwango kikubwa kwenye uzalishaji wa saruji mkoani Mtwara, alikutana na Rais Samia Suluhu Hassan hivi karibuni na kumwahidi kuwekeza pia kwenye uzalishaji wa mbolea.

Mkurugenzi wa TIC alisema tayari kituo hicho na wadau wengine wa sekta ya uwekezaji wameshakaa na kuandaa ardhi ya kutosha kwaajili ya kumpatia Dangote eneo ambalo atajenga kiwanda kikubwa cha mbolea.

Alisema wamemtafutia maeneo wilayani Lindi na Mtwara ambako kutakuwa na miundombinu mizuri kama barabara na ambako kutakuwa rahisi kwake kuingiza gesi kwenye kiwanda hicho kutoka Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC).

"Dangote alipokutana na Rais Samia hivi karibuni pamoja na mambo mengine alimweleza nia yake ya kuwekeza kwa hiyo na sisi kwa kuzingatia uwekezaji mkubwa aliofanya kwenye saruji tumekaa na wadau kuangalia maeneo ya kumpa kwaajili ya kumvutia kufanya uwekezaji huo," alisema.

"Ardhi ipo tayari kwa Mkoa wa Lindi, Wilaya ya Kilwa ambako kuna maeneo makubwa matatu anaweza kuwekeza, Pwani kuna maeneo mawili tunaamini kwa ardhi atapata kubwa na kwa haraka," alisema.

Aidha, mkoani Mtwara kuna maeneo kadhaa ambayo hawajapata vipimo, lakini yapo wanaamini mwekezaji huyo atapata ardhi ya kutosha kuwekeza.

Kuhusu gesi alisema wamezungumza na TPDC ambao wamemhakikishia mwekezaji huyo kuwa atapata gesi ya kutosha kadri atakavyohitaji na kilichobaki ni kukutana naye kusikiliza mahitaji yake mengine.

Alisema miundombinu kuelekea mikoa hiyo iko vizuri na kuna umeme wa uhakika na maji na kuwa rahisi kwa uwekezaji wa aina yoyote atakaohitaji kuufanya.

"Tumendandikia barua ya kuomba kukutana naye hivyo tunasubiri tarehe tu atakayotuambia kwamba yuko tayari ili twende Mtwara kukutana naye na tutaenda na wadau mbalimbali wanaohusika na uwekezaji hasa kwenye sekta ya mbolea," alisema.

Alisema uwekezaji huo utakuwa na manufaa makubwa kwa Tanzania kwa kuwa mwekezaji huyo atatosheleza soko la ndani na kuuza nchi za nje na kusaidia kuinua uchumi wa nchi kwa kulipa kodi na kuongeza ajira kwa Watanzania.

# Wananchi kupewa mafunzo ya sheria

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

KITUO cha Msaada wa Kisheria Kibaha (KPC) kinatarajia kuwafikia watu takriban 40,000 katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha kuwapatia elimu ya msaada wa kisheria.

Tayari kituo hicho kimewajengea uwezo viongozi wa serikali za mitaa na kutoa elimu ya kisheria kwa wananchi kwenye Kata ya Tumbi.

Katibu wa kituo hicho, Dismas Chihwalo, aliiambia Nipashe jana kuwa wamewajengea uwezo viongozi hao kuhusiana na masuala ya sheria mbalimbali ili wawasaidie wananchi na kuwaelekeza njia za kufuata kupata haki zao.

Chihwalo alisema wameanza kwa viongozi kwa kuwa wao ndiyo watu wa mwanzo kupata taarifa za masuala yanayokwenda kinyume cha sheria kutoka kwa wananchi wanaowaongoza.

Katibu huyo alisema wanatoa pia elimu na msaada wa kisheria kwa wananchi ili kutatua migogoro kabla ya kufika kwenye vyombo vya kisheria au baada ya kufika huko.

Alisema kuwa mbali ya kuwajengea uwezo viongozi wa kata na mitaa, pia wamefikisha elimu ya msaada wa kisheria kwa wananchi, wakiwamo wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mwanalugali na Shule ya Msingi Tumbi kuhusu Sheria ya Mtoto na makundi ya vikoba kwenye Kata ya Tumbi.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Mwanalugali, Deo Rwekaza, alisema mafunzo hayo yanawasaidia kuwahudumia wananchi wanapofika ofisini wakiwa na malalamiko na migogoro ambayo huwa wanawaelekeza njia nzuri ya kuwasaidia kuitatua.

Rwekaza alisema kuwa baadhi ya wananchi wanapokuwa na migogoro, wanakuwa hawajui cha kufanya au hatua za kufuata.

# Serikali yageukia ubaguzi, unyanyapaa katika hedhi

**Na Enock Charles**

SERIKALI imesema elimu ya kupinga unyanyapaa na ubaguzi kwa wasichana na usafi wa msichana wakati wa hedhi inahitajika katika shule za msingi, sekondari na jamii ili kuwa na kizazi bora.

Imesema elimu hiyo itasaidia wasichana kuepuka udhalilishaji na kuwa na hedhi salama.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Dk. Joyce Nyoni, aliyemwakilisha Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mwanaidi Khamis, katika hafla ya kukabidhi msaada wa taulo za kike kwa wasichana wa shule za msingi na sekondari za Mkoa wa Dar es Salaam zilizotolewa na Kampuni ya KEDS Tanzania.

"Ni asilimia 28 tu ya wasichana wana ufahamu mzuri kuhusu hedhi, walio wengi bado wanakabiliwa na changamoto ya kumudu usafi, upatikanaji wa maji safi na salama pamoja na vyoo vyenye afya," alisema.

Dk. Joyce alisema wasichana wakati wa hedhi wanakabiliwa na vikwazo vingi pamoja unyanyapaa na ubaguzi, hivyo ni wakati wa kuacha tabia kama hizo ili kusaidia wasichana kupata elimu yao kwa uhuru.

Mkurugenzi wa KEDS Tanzania Limited, Victor Zhang, aliunga mkono na kujitolea katika kuhakikisha kuwa wasichana wanakuwa salama siku za hedhi na hawapotezi tabasamu zao wala usingizi wao kwa sababu ya hedhi kutokana na unyanyapaa unaoweza kusababishwa na msichana kutokuwa safi wakati wa hedhi.

Zhang alisema KEDS Tanzania inasimama na serikali katika harakati za uwezeshaji wa wasichana na wanawake nchini na inaamini siku zijazo zitapatikana njia bora za kufikia malengo kwa wasichana na njia sahihi ni kuanza kuwaunga mkono wakiwa shuleni ili wasome kwa bidii na kufikia ndoto zao.

"Tunataka kuona wasichana nchini wakiishi ndoto zao kwa kusoma kwa bidii bila kukosa masomo yao kutokana na hedhi.

"Tunataka kuhakikisha kwamba msichana aliye na ndoto kuwa rubani, hakosi nafasi hiyo kwa kushindwa kumaliza masomo kutokana na hedhi isiyo salama.

"Msichana ambaye ana ndoto ya kuwa daktari, vilevile asipoteze nafasi hiyo," Zhang alifafanua.

Akizungumza kwa niaba ya shule zingine za sekondari, Dada Mkuu wa Shule ya Sekondari Zanaki, Siti Othman, alisema wasichana wengi wamekuwa wakikosa masomo wakati wa hedhi kwa kuhofia kudhalilishwa.

Siti alibainisha kuwa udhalilishaji huo unasababisha wawe nyuma kielimu kulinganishwa na wavulana, jambo ambalo aliiomba jamii na serikali kuwapigania.

"Kwa niaba ya wasichana wenzangu, ningewasihi wadau wengine wawaunge mkono wasichana kwa kutoa usafi wa mazingira kwa sababu wanatusaidia sana katika elimu yetu," alisema Siti.

KEDS Tanzania Limited ilitoa msaada wa pedi 14000, sabuni za kunawia na vifaa vingine vyenye thamini ya Sh. milioni 30 kwa shule 21 za Mkoa wa Dar es Salaam zikiwamo Shule za Sekondari, Zanaki, Jangwani, Tambaza, Kisutu na Dar es Salaam.



Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la WWF, Dk. Aman Ngusam (kulia), Mkurugenzi wa Vodacom Foundation Rosalynn Mworia (katikati) na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), Prof Dos Santos Silayo wakishirikiana kupanda mti katika eneo la Medeli, jijini Dodoma jana, ikiwa ni sehemu ya shamrashamra kuelekea siku ya kimataifa ya mazingira duniani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC aonya wapotoshaji matibabu ya kichocho

**Na Neema Sawaka, KAHAMA**

MKUU wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, Annamringi Macha, amewataka wananchi kuacha kuzusha uvumi kuwa dawa za kinga na tiba ya minyoo na kichocho wanazonyweshwa wanafunzi wa shule za msingi ni kinga ya virusi vya corona.

Amesema uvumi huo unasababisha kukwamisha utoaji wa huduma hiyo wilayani mwake.

Akizungumza na Nipashe jana, Macha alisema wanafunzi wanaopewa dawa hizo ni wa shule mbalimbali za msingi katika Manispaa ya Kahama, Halmashauri za Ushetu na Msalala wilayani hapa.

Dawa hizo ni mahususi kukinga na kutibu minyoo na kichocho ili kuzuia magonjwa hayo ambayo ni hatari kwa watoto.

Kiongozi huyo wa wilaya aliyasema hayo alipozindua mpango rasmi wa serikali wa dawa za kichocho na minyoo kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Majengo iliyopo Manispaa ya Kahama.

Alisema wapo watu wanaozusha uvumi kwamba hiyo ni dawa ya kinga ya corona na kuongeza kuwa serikali ipo makini na haiwezi kuangamiza watu wake.

Alitumia nafasi hiyo kuwaonya na kuahidi kuchukua hatua dhidi ya wanaoeneza uvumi kuwapotosha wenzao.

"Ndugu zangu dawa hizi ni kwa ajili ya kuhakikisha kuwa watoto wetu wanajikinga na magonjwa ambayo yalikuwa hayapewi kipaumbele wakati mwingine wanaweza kukondeana.

"Mtoto anakula chakula na minyoo nayo inakula, kwa hiyo unaweza kudumaa na ukadumaza akili, wataalamu wanasema inaweza hata kukusababishia kifo," alisema.

"Shule ya Msingi Majengo ni miongoni mwa shule 114 zenye jumla ya wanafunzi 3,510. Kati yao, 3,424 watapata dawa hizo za minyoo na kichocho.

"Hatuna sababu yoyote ya kupata matatizo ya magonjwa ambayo uwezo wa kuyatibu tunao," alisema.

Mkuu wa wilaya huyo aliwaeleza wazazi kuwa ili kudhibiti magonjwa hayo, wazazi wanapaswa kuzingatia watoto kuvaa viatu kwa kuwa kutovaa viatu kwa kuwa ni kutokuvaa ni njia hatarishi ya maambukizi hayo na kuwasisitiza walimu nao kuzingatia suala la usafi katika vyoo.

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Manispaa ya Kahama, Dk. Lucas David, alibainisha lengo la manispaa ni kuwafikia walengwa 88,907 wanaostahili kupata dawa za minyoo na kichocho katika shule 114.

"Kwa ushirikiano wa walimu na wahudumu wa afya waliopo, zoezi litakwenda vizuri kama lilivyo agizo la serikali, niwaombe wazazi tuendelee kuruhusu watoto wetu waje kupata kinga na tiba hii

# 'Uchunguzi wa awali mtoto alikufa kwa malaria kali'

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

POLISI mkoani Kagera inaendelea kuchunguza kifo cha mtoto Boniface Bernard (6), mwanafunzi wa darasa la awali katika kituo cha Magereza, ambaye inadaiwa na majirani kuwa ameuawa na mama yake kwa kumnywesha sumu, hata hivyo, imesema kinacholeta shaka huenda taarifa hizo sio za kweli.

Akizungumzia tukio hilo Kamanda wa Polisi mkoani Kagera, Revocatus Malimi, alisema walipokea taarifa Mei 30, mwaka huu, kutoka kwa majirani wa mama mzazi Evodia Andrew (25) wa mtoto huyo wakidai kumuua mtoto wake kwa sumu na kuanza uchunguzi.

"Uchunguzi wa awali umeonyesha kuwa mtoto huyo alikufa baada ya kuugua malaria kali na kupelekwa katika zahanati ya Buyekera inayomilikiwa na polisi, akapatiwa matibabu na kuruhusiwa, tunaendelea na uchunguzi lakini inaonekana kama ni taarifa za uzushi," alisema.

Alisema kuwa kinacholeta shaka kuwa huenda taarifa hizo sio za kweli, tukio la kumpa sumu mtoto majirani hao wanadai lilifanyika tangu Mei 10, mwaka huu na mtoto kufariki siku mbili baadaye, na kuhoji kwa nini wananchi walikaa muda mrefu bila kutoa taarifa polisi.

Alisema wananchi wanne waliotoa taarifa na maelezo yao kuchukuliwa, mmoja wao Lydia Respicius, alidai alimshuhudia mama huyo akimnywesha sumu mtoto wake, lakini baadaye alipohojiwa na polisi alikana. "Wananchi hao wametishia kujichukulia sheria mkononi wakishinikiza mama huyo ahame katika mtaa huo, lakini nawaonya wasijaribu kufanya hivyo vinginevyo watakumbana na mkono wa sheria, kwa kuwa uchunguzi unaendelea unapaswa kuwa na subira," alisema.

Alisema kuwa mama huyo anayetuhumia kumuua mwanawe alikamatwa na kuhojiwa na kisha kuachiwa kwa dhamana.

"Endapo italazimika kufanya uchunguzi zaidi upo utaratibu wa kisheria unaotumika, tutaomba kibali kufanya hivyo, lakini hadi sasa bado ni taarifa ambazo kwetu hazina mashiko," alisema Kamanda Malimi.




Meneja wa Tigo Kanda ya Kaskazini, Daniel Mainoya (kushoto), akipokea moja ya miche ya miti 7,000 kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Helios Towers Tanzania, Ramsey Koola, wilayani Hai, mkoani Kilimanjaro jana, kwa ajili ya kuchangia kampeni ya upandaji miti eneo la Mlima Kilimanjaro ya Tigo Green For Kili. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia kushiriki mkutano wa nne kiuchumi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kushiriki mkutano wa nne kiuchumi na maombi ya kitaifa ambao unalenga kujadili masuala ya utawala bora na uadilifu katika uongozi.

Mkutano huo utafanyika Juni 12, mwaka huu, jijini Dodoma na utajumuisha viongozi mbalimbali wa serikali, vyama vya siasa, taasisi za kibiashara za ndani na nje na madhehebu mbalimbali ya dini.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi ya Kingdom Leadership Network Tanzania (KLNT), Isaac Mpatwa, alisema mojawapo ya misingi muhimu ya maendeleo ya kiuchumi yanayowajali maskini, utawala bora ni nguzo ya mtazamo wa kitaifa wa maendeleo.

"Kutakuwapo na maombi na tunalenga kuwakumbusha na kuwalea viongozi wa kitaifa waadilifu, wazalendo na wanaomuogopa Mungu," alisema.

Mpatwa alisema Msemaji Mkuu katika tukio la mwaka huu ni Dk. Bill Wiston, ambaye ni kiongozi mashuhuri na mfanyabiashara mkubwa aliyefanikiwa nchini Marekani.

"Tunatarajia kujumuisha viongozi 500 wa kiserikali, siasa, wabunge, wafanyabiashara, wawakilishi wa balozi mbalimbali, viongozi wa dini na wananchi," alisema.

Pia, alisema KLNT watazindua kituo cha kulelea wafanyabiashara pamoja na jukwaa maalum la wafanyabiashara wa Tanzania na Marekani litakalofanyika mwishoni mwa mwaka huu na kuibua fursa mpya za biashara na uwekezaji baina ya wafanyabiashara wa nchi hizo.

Alisema tangu kuanza kufanyika kwa mikutano hiyo nchini kumekuwa na mafanikio makubwa ikiwamo kutoa mafunzo kwa viongozi masuala ya utawala bora na uadilifu.

# Wanafunzi 100 wadaiwa kulala chumba kimoja

**Na Zuhura Zukheir,** IRINGA

WANAFUNZI zaidi ya 100 wanadaiwa kulala chumba kimoja Shule ya Sekondari Ketewaka, Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, kutokana na upungufu wa mabweni, hali inayosababisha kuambukizana magonjwa ya ngozi.

Akizungumza na waandishi wa habari Mwalimu Mkuu wa Shule ya Kitewaka, Mosela Mgaya, alisema uwezo wa bweni ni kukaa wanafunzi 45, lakini kwa sasa wanafunzi wanaotumia bweni hilo ni 125 hali inayochangia kwa kiasi kikubwa kuambukizana magonjwa ya mlipuko.

Alisema tatizo hilo ni kilio kikubwa cha wanafunzi wa shule hiyo kutokana na shule kuwa na bweni moja lenye uwezo wa kubeba wanafunzi 48 na sasa wamelazimika kuwaweka wanafunzi zaidi ya 100 hali inayohatarisha afya zao.

Alisema ili kuwaepusha wanafunzi wasichana kukutana na tatizo la kukatishwa masomo kwa kushawishiwa na kupata ujauzito, walilazimika kuwaweka wasichana bwenini.

Mgaya alisema kuwa mrundikano huo wa wanafunzi katika bweni moja unachangia kwa kiasi kikubwa wanafunzi kuambukizana magonjwa ya ngozi na kwa sasa robo ya wanafunzi wanaolala katika bweni hilo wameanza kuugua ugonjwa huo.

Fidea Steven na Steria Haule, wanafunzi wa shule hiyo, walikiri kukabiliwa na tatizo hilo na kuiomba serikali na wadau wa elimu kuwasaidia kujenga bweni lingine litakalo waondolea adha ya mrundikano na magonjwa ya kuambukiza.

Mbunge wa Jimbo la Ludewa, Joseph Kamonga, aliyetembelea shule hiyo, alisema ameziona changamoto za bweni, ukarabati wa madarasa na atalifikisha katika Baraza la Madiwani na kutafuta wadau watakaoweza kusaidia ujenzi wa mabweni na ukarabati wa vyumba vya madarasa.

Alisema kuwa vyumba vya madarasa vya shule hivyo havina madirisha hali inayohatarisha afya za wanafunzi kutokana na baridi kali linalotokana na jiografia ya jimbo lake na Mkoa wa Njombe kuwa na baridi kali.

Pia uhaba wa mabweni na ubovu wa vyoo, ukosefu wa maji ya uhakika na vitabu vya kiada na ziada jambo linalorudisha nyuma kiwango cha elimu shuleni hapo.

# Bil. 1/- kujenga kongano la kubangua korosho

SERIKALI imetenga Sh. bilioni moja kwa mwaka wa fedha 2021/22 kwa ajili ya ujenzi wa kongano la kubangua korosho eneo la Masasi.

Kongano hilo litasaidia ubanguaji wa korosho kwa maeneo yote ya Masasi na Newala.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti maalum (CCM), Agness Hokororo.

Katika swali lake, Mbunge huyo alitaka kujua kama serikali itafufua viwanda vya korosho vilivyopo katika wilaya za Masasi na Newala ili kuchakata korosho ghafi na kuongeza bei ya zao hilo.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema wilaya za Masasi na Newala zilikuwa na viwanda vitatu vya kubangua korosho vilivyokuwa vikimilikiwa na serikali na hatimaye kubinafsishwa.

"Viwanda hivyo ni Masasi Cashew Factory, Newala I Cashew Factory na Newala II Cashew Factory," alisema.

Alisema kiwanda cha korosho cha Masasi kilibinafsishwa na kuuzwa kwa Kampuni ya BUCCO Investments Holdings Limited ambayo ilishindwa kukiendesha kutokana na Benki ya CRDB kuzuia mali za kiwanda baada ya kushindwa kurejesha mkopo.

"Hatimaye kiwanda kiliuzwa na Benki ya CRDB kwa Kampuni ya Micronix Export Trading Co. Ltd kwa njia ya mnada, Kampuni ya BUCCO Investments Holdings Limited, hawakuridhika na utaratibu uliotumika kuuza kiwanda hicho, walifungua kesi mahakamani na kuishtaki Benki ya CRDB na kesi hiyo bado ipo mahakamani hivyo uendelezaji wa kiwanda hicho umesimama kusubiri maamuzi ya mahakama," alisema.

Alisema kiwanda cha Newala I Cashew Factory kilinunuliwa na Kampuni ya Micronics System Ltd na kinaendelea kufanya kazi na Kiwanda cha Newala II Cashew Factory kilinunuliwa na Kampuni ya Agrofocus (T) Ltd.

"Tangu kibinafsishwe, kiwanda hicho hakijawahi kufanya kazi, hivyo mwaka 2019 kilirudishwa katika umiliki wa serikali chini ya Ofisi ya Msajili wa Hazina, kiwanda hicho kama vilivyo viwanda vingine vilivyorudishwa serikalini kipo katika utaratibu wa kupatiwa mwekezaji mwingine mwenye uwezo wa kukiendeleza," alisema.

Hata hivyo, alisema kwa kutambua umuhimu wa kuendeleza sekta ya viwanda wilayani Masasi na Newala, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, serikali imetenga Sh. bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa kongano la kubangua korosho eneo la Masasi.

"Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo pamoja na Sekta Binafsi inaendelea kuweka mazingira ya ufufuaji na ujenzi wa viwanda nchi nzima ikiwamo maeneo ya Masasi na Newala," alisema.



Waziri Mkuu, Kasimu Majaliwa (kulia), akijadiliana jambo na Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani (kushoto) na Naibu wake, Stephen Byabato, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Barabara Kilosa-Mikumi yatafutiwa fedha

WIZARA ya Ujenzi na Uchukuzi, imesema inaendelea na utafutaji wa fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya barabara ya Kilosa hadi Mikumi yenye urefu wa kilometa 73.3.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Godfrey Kasekenya, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti maalum (CCM), Dk. Christine Ishengoma, aliyetaka kujua mkakati wa serikali wa kujenga barabara ya kiwango cha lami kuanzia Kilosa hadi Mikumi. Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kasekenya, alisema barabara ya Kilosa hadi Mikumi ni sehemu ya barabara ya Dumila - Rudewa - Kilosa - Mikumi yenye urefu wa kilometa 142.3 ambayo ni ya mkoa inayosimamiwa na wizara kupitia Wakala wa Barabara nchini (TANROADS).

"Serikali inaendelea na ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kwa awamu ambapo ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya barabara kutoka Dumila hadi Rudewa yenye urefu wa kilometa 45 ulishakamilika na barabara inatumika," alisema.

Alisema ujenzi wa kiwango cha lami wa sehemu ya barabara kutoka Rudewa hadi Kilosa yenye urefu wa kilometa 24 ulianza Februari, 2019 na unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2021.

"Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa sehemu ya barabara iliyosalia kutoka Kilosa hadi Mikumi yenye urefu wa kilometa 73.3 kwa lengo la kujenga kwa kiwango cha lami imeshakamilika," alisema.

## Sababu kuanzishwa hifadhi Kitulo zatajwa

BUNGE limeelezwa sababu nne zilizosababisha serikali kuanzisha Hifadhi ya Taifa ya Kitulo.

Naibu Waziri ya Maliasili na Utalii, Mary Masanja, alitoa kauli hiyo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Busokelo (CCM), Atupele Mwakibete.

Alihoji serikali haioni umuhimu wa kuwapa wananchi maeneo ya Hifadhi ya Taifa Kitulo ambayo hayatumiki ili kulisha mifugo yao hususani eneo la Kwipanya.

Akijibu, Masanja alisema Hifadhi ya Taifa Kitulo ilianzishwa kwa GN. Na.279 ya mwaka 2005 na maeneo yote yaliopo ndani ya hifadhi hiyo likiwamo eneo la Kwipanya, yamehifadhiwa kisheria kulingana na umuhimu wake kiikolojia, kijamii, kitamaduni na kiuchumi.

"Miongoni mwa sababu za serikali kuanzisha hifadhi hii ni pamoja na kuhifadhi vyanzo vya maji ambavyo vinatoa maji yanayoenda kwenye Bonde la Nyasa na Bonde la Rufiji, kwa sasa maji hayo yanachangia kwenye miradi mikubwa ya kimkakati ikiwamo Mradi wa kufua umeme wa maji uliopo katika Bwawa la Julius Nyerere pamoja na bwawa la kufua umeme wa maji la Mtera," alisema.

Alitaja sababu nyingine kuhifadhi uoto adimu wa asili wa misitu na maua uliopo katika eneo husika, kutunza makazi ya wanyama adimu duniani kama vile Kipunji na Minde na kuhifadhi mandhari ya asili ya milima kwa ajili ya shughuli za utalii.

"Serikali itaendeleea kuhifadhi eneo la Hifadhi ya Taifa Kitulo kutokana na umuhimu wake," alisema.

Katika maswali ya nyongeza, alihoji serikali ina mpango gani wa kurekebisha mipaka ili iwe na uhalisia.

"Hifadhi ya Kitulo inajulikana kama bustani ya Mungu kwa sababu ina maua ya kipekee na hifadhi pekee Afrika ina maua mazuri sana lakini haijatangazwa, serikali ina mpango gani wa kutangaza ili ijulikane," alihoji.

Naibu waziri, Masanja aliahidi kwenda na wataalamu kuangalia mipaka inayodaiwa kukosewa katika hifadhi hiyo.

Alisema bajeti ya mwaka 2021/22 ya wizara hiyo imezingatia mambo mbalimbali ikiwamo kuitangaza kwa nguvu zote hifadhi hiyo.




Habari zote na Augusta Njoji



Ukurasa 13

Soma madarasa yote jirudie nyumbani

BUFE
IJUMAA JUNI 4, 2021
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA


Ukurasa 14

**AGRI-CONNECT**
**Mradi ulioibua mavuno mapya kahawa, maisha mapya walimaji Nyanda za Juu**

BIASHARA

## KWANINI MAFUTA YA KULA BEI JUU?

# Huu hapa uhalisia wanaoibua mawaziri, vigogo wanaoshikilia kona zote kisekta

•Wizarani, viwadani, watafiti, madukani...
•Sababu ya shehena iliyoagizwa kupwaya

**Na Christina Mwakangale**

KATI ya bidhaa muhimu kwa matumizi ya mlo wa binadamu kila siku, mafuta ya kupikia ni mojawapo na wakati mwingine matumizi yake hayaepukiki.

Katika mapishi aina yeyote, mafuta hutegemewa kama kiungo muhimu au kianzio cha lazima katika kuunga mboga, kuangua vitoweo, kuoka, la sivyo kinachopikwa kikikosa mafuta uwezekano wa kuungua kukiwa motoni ni mkubwa.

Kwa kipindi cha miezi mitatu au minne mfululizo bidhaa hiyo imeadimika maeneo mengi nchini na yanakopatikana bei yake haikamatiki.

Nipashe imebaini katika mikoa tofauti nchini, bei ya bidhaa hiyo imeendelea kuwa juu madikani, licha ya serikali kufanya jitihada kuletea shehena kubwa ya bidhaa hiyo.

Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, akiwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya wizara, bungeni Dodoma, anasema serikali inakuja na mkakati kukabiliana na uhaba na kupanda bei ya mafuta nchini, kwa kuanza kutumia mbegu mpya za alizeti na kuhamasisha kilimo cha michikichi.

Wakati waziri anasema hayo, wadau wa bidhaa hiyo wakiwamo wafanyabiashara na taasisi wanaeleza hali iliyosababisha bei kupanda, ni kutozingatiwa ushauri muda mrefu walioutoa.



Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

### HALI HALISI

Mwenyekiti wa Chama cha Wasindikaji Mafuta ya Alizeti Tanzania (TASUPA), Ringo Iringo anasema asilimia 80 hadi 90, ya mchikichiki, inayolimwa zaidi mkoani Kigoma imekwishazeeka, ikiwa na umri hadi miaka 60 sasa

"Uzalishaji wenye tija ni miaka 30 miti iliyopo sasa imezeeka. Kuna hekta laki nne kilimo hiki nchini lakini inayotumiwa ni hekta 30,000 tu," anasema Ringo na kuongeza:"Asilimia 90 imezeeka miti ya michikichi huzaa Mawese. Ardhi uliyotuma kwa michikichi ni ndogo."

Anashuari kutumika mbegu za kisasa za michikichi zitakuza kilimo chenye tija kitakachosaidia kupunguza uhaba wa mafuta, ambao kwa kiasi kikubwa umeegemea zaidi alizeti inayopatikana kwa shida hata baadhi ya viwanda kufungwa.

"Kilimo cha alizeti kwa wakulima wengi ni kama mazoea tu si rasmi, utakuta kwenye shamba la mahindi ndio inalimwa alizeti chache tu. Yawapo maeneo na mashamba rasmi, ili kukabiliana na kupanda bei na uhaba wa mafuta ya kupikia," anafafanua.

Anasema kwamba katika viwanda 770 nchini, vinahitaji zaidi ya tani 4,000 kwa siku kukidhi mahitaji ya malighafi, lakini hayapatikani ya kutosha.

Ringo anasema mara kadhaa walitoa wito kwa serikali kuweka mkakati wa kuboresha mbegu bora, tangu mwaka 2016, lakini haujatekelezwa ipasavyo.

"Serikali itoe maeneo ya kilimo cha mazao yanayozalisha mafuta. Hivi sasa tunapata hasara, hakuna mbegu za kukamua mafuta ili yasindikwe. Wakulima wetu hawazalishi kitaalamu bali kwa kutatua tatizo lake, chakula, ada yaani atatue shida zake na si tija yaani kibiashara."

Ringo anabainisha hivi sasa kuna viwanda viwili pekee vya alizeti nchini, ndiyo vinavyoendelea na uzalishaji, vingine vimefungwa kutokana na uhaba wa malighafi na wanatarajia kuvifungua, mavuno yatakapoongezeka.

"Uzalishaji alizeti umeanza ndio utaona viwanda vingine vinaanza kufunguliwa. Mfano kiwanda kimoja uwezo ni kuwa na tani 100 za alizeti ili kukamua, hakuna mkulima anazalisha kiasi hiki. Viwanda vingi vinasuasua," anasema Ringo.

Kutokana na hilo, anasema imechangia ajira kupungua na uwekezaji kushuka na kwamba mafuta hayajaadimika kwa mahitaji ya majumbani pekee, bali viwandani kunakohitajika kusindikia vyakula mbalimbali.

### WATAFITI TARI

Mtafiti wa zao la mchikichi kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Dk. Folsom Kagimbo,

INAENDELEA UK.12

BIASHARA

## KWANINI MAFUTA YA KULA BEI JUU?

# Huu hapa uhalisia wanaoibua mawaziri, vigogo wanaoshikilia kona zote kisekta

INATOKA UK.11

anasema kupitia kituo cha utafiti Kihinga, mkoani Kigoma umeanza kuzalisha mbegu bora na kugawa bure

Anafafanua Dk. Kagombo:"Shida ya wakulima wa michikichi hawatumii kanuni bora, hivyo tunatoa elimu."

Pia, anataja tatizo la walima michikichi Kigoma wamerithi mashamba ya muda mrefu na ulimaji wao hawafuati kanuni stahiki, ingawa anakiri kuwapo sura ya pili baadhi ya wakulima wanatumia mbegu za kisasa.

**WALIMA MBEGU**

Dk. Sophia Kilenga, Mtendaji Mkuu Wakala wa Mbegu Bora za Kilimo (ASA), anaorodesha matatizo ya mazao ya mafuta kusuasua, kwamba ni; utuimiaji kanuni na mbegu duni, pia upotevu katika mavuno na elimu inayopwaya.

"Hekta moja uzalishaji ni 0.4 tani (kilo 400) kwa hekta, uzalishaji ukiwa wa tija itafikia 0.7 (kilo 700) kwa mbegu ya alizeti. Michikichi hadi ianze kutoa mavuno ni miezi 18 tangu kupandwa hadi kuzaa.

"Upotevu ni kukosa vifaa vya kuvunia, asilimia 40 ya mavuno hupotea kuanzia shambani hadi nyumbani. Tani 167,000 za mbegu ni mahitaji yanayohitajika, ila uzalishaji ni tani 67,000 pekee kwa sasa," anaeleza

**TBS**

Kaimu Mkuu wa Ukaguzi na Ufuatiliaji kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Athumani Kisumo, anataja janga la maradhi corona, ilichangia nchi wazalishaji kupunguza.

'Tulitarajia mafuta shehena kuwasili Mei 27, mwaka huu. Kuingia nchini inafahamika bei 'ime-double' (ongezeka bei mara mbili) tangu mwaka jana," anasema Kisumo.

**HALI HALISI**

Uhaba wake madukani unatajwa kuchangia bei ya bidhaa hiyo kutoshuka na hivi sasa baadhi ya wananchi wamebadili utamaduni kwa kutumia mbadala wa karanga na nazi kwenye mlo.

Uchunguzi wa Nipashe umebaini katika baadhi ya mikoa bei imeendelea kuwa juu, licha ya jitihada za serikali kuingiza nchini shehena ya bidhaa hiyo.

Ally Omar na Karim Magwila, wenye maduka ya rejareja katika Barabara ya 15 jijini Tanga, wanasema bei ya mafuta inaendelea kupaa kutokana na uhaba wake.

Omar anasema, penye ujazo wa lita moja, hivi sasa inauzwa kwa bei Sh. 5,000, huku katoni yenye lita 12 ikiuzwa Sh. 54,000, wakati awali lita moja iliuzwa Sh. 3,000 hadi Sh. 3,500.

Pia, anasema mafuta ya ujazo wa lita tatu yanauzwa kwa Sh. 15,000 na katoni yenye chupa sita huuzwa Sh. 86,500, ndoo yenye ujazo wa lita 10 inauzwa Sh. 43,500 kwa rejareja na jumla ni Sh. 42,800.

Hali kadhalika wiki iliyopita mkoani humo, lita moja ya alizeti ili kwa Sh. 7,500 huku katoni yenye chupa 12 ikiuzwa Sh.78,000, ujazo wa lita tatu ikiuzwa Sh. 20,000 na Sh. 109,000 kwa katoni yenye chupa sita.



Mchikichi ukivunwa shambani. Chini kulia, mafuta mawese yakiandaliwa.





Mafuta ya kula katika ngazi tofauti za uzalishaji na matumizi.

**KILIMANJARO**

Wafanyabiashara ndogo katika soko la Lawate, wilayani Siha, wanasema bei haijashuka, awali mafuta ya kula ya ujazo wa lita tatu yaliuzwa kwa Sh. 16,000 na sasa yanauzwa Sh. 24,000, huku lita tano iliyokuwa ikiuzwa Sh. 20,000 inauzwa Sh. 32,000 hadi Sh. 34,000.

Mfanyabiashara Erick Mlay, anasema kwa sasa lita moja ya mafuta inauzwa 6,000, huku lita tatu ni Sh. 18,000 na lita tano kwa Sh. 35,000.

**SHINYANGA**

Katika soko kuu mkoani Shinyanga, nako kunaripotiwa bei ya mafuta haijashuka tangu Januari iliyopita; lita moja ya mafuta ya kula iliuzwa Sh. 4,000 na sasa Sh. 5,000; lita tano ni Sh. 25,000 kutoka bei ya awali Sh. 23,000.

Inabainishwa kwamba lita 20 inauzwa kwa Sh. 85,000, wakati mwezi Januari iliuzwa Sh. 77,000; wilayani Kahama bei ya lita 20 inauzwa Sh. 85,000 kutoa bei ya awali Sh. 83,000.

Pia, mafuta ya kula lita 10 kwa sasa inauzwa Sh. 45,000 na awali iligota Sh. 23,000.

**MWANZA**

Jijini Mwanza, bei imepanda ndoo ya lita 20, inauzwa Sh. 83,000 badala ya Sh. 58,000 ilivyokuwa miezi miwili iliyopita.

Ujazo wa mafuta lita tano ilikuwa Sh. 20,000, sasa ni Sh. 27,000. Mafuta ya lita tatu yaliyouzwa Sh. 12,000, sasa bei ni Sh. 16,000; lita moja ya alizeti inauzwa Sh. 7000 badala ya Sh. 6000 na kuna aina nyinginezo kuuzwa Sh. 5,000 badala ya Sh. 4500.

**KAGERA**

Mjini Bukoba, mafuta alizeti ujazo wa lita tano yanauzwa Sh. 30,000 badala ya Sh. 17000, mwanzoni mwa mwaka huu; lita 20 yanauzwa Sh. 115,000 badala ya Sh. 85,000 na lita tano yanauzwa Sh. 26000 badala ya Sh. 18,000, huku ujazo wa lita 20 yanauzwa Sh. 104,000 badala ya Sh. 90,000.



**DODOMA**

Jijini Dodoma kunatajwa kuwapo afueni ya bei, baada ya kushuka kutoka Sh. 7,000 kwa lita moja ya mafuta ya alizeti hadi Sh. 5,000.

Mmoja wa wasindikaji wa mafuta ya alizeti jijini humo, Selina Kuziganika, anasema kushuka huko kwa bei kunachangiwa na kuanza msimu wa mavuno ya alizeti.

Anasema, ni hali inayochangiwa na kuongeka uzalishaji ulioshuka awali, hata hivyo, Nipashe imegundua bei zinatofautiana kutokana na ubora wa mafuta. Yapo yanayouzwa hadi Sh. 38,000 kwa lita tano.

**MBEYA**

Jijini Mbeya, Nipashe imegundua bei kuanza kushuka kutoka Sh. 130,000 na 140,000 kwa lita 20 kuanzia Aprili mwaka huu, hadi Sh. 100,000 na 120,000, mwezi huu (Mei), kutokana na ongezeko la alizeti.

Wafanyabiashara wa bidhaa hiyo, wanasema bei imeshuka kutokana na mavuno ya alizeti katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kuongezeka.

Mjasiriamali wa mafuta katika eneo la Sokoine, jijini Mbeya, Subira Mwakyoma, anasema mwezi Aprili lita moja waliuza kati ya Sh. 7,000 na 7,500 na sasa imeshuka na kufikia kati ya Sh. 5,000 na 6,000.

"Kwa sasa ukienda kwenye mashine tunanunua Sh. 100,000 na tukija huku mtaani tunauza kwa bei tofauti, binafsi nauza lita moja Sh. 6,000," anasema Subira.

**MANYARA**

Wauzaji wa mafuta ya alizeti mkoani Manyara, wanasema bei imeanza kushuka kwa sababu inavunwa sasa.

Mkamuaji mafuta, Africans Panga, anasema wanauza dumu moja la lita 20 kwa Sh. 70,000 na dumu la lita tano Sh. 20,000. Awali lita tano liliuzwa Sh. 27,000 na lita 20 Sh. 110,000.

**ARUSHA**

Maduka kadhaa jijini Arusha, yalikuwa yakiuza mafuta ya kula bei juu kwa zaidi ya miezi mitano sasa.

Katika baadhi ya maduka mafuta aina ya safi ya ujazo wa lita 10 yaliuzwa Sh. 38,000 mwezi Julai mwaka jana na lita 20 yaliuzwa Sh. 77,000.

Pia, kuna mafuta bora ya alizeti ya lita tatu yanauzwa kati ya Sh. 18,000 hadi 20,000 na lita tano yanauzwa Sh. 20,000.

**NASAHA SERIKALINI**

Waziri Mkenda, anasema ili kupunguza uhaba wa mafuta kuna haja ya kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula.

"Wizara itaendelea kueneza mbinu ya kilimo cha mkataba iliyoanza kutumiwa na baadhi ya wenye viwanda kama vile Pyxus ili kuchochea uzalishaji na uhakika wa soko kwa mkulima.

"Katika mwaka 2021/2022, wizara itahamasisha uzalishaji wa chikichi kufikia tani 50,000 na alizeti kufikia tani 1, 000, 000," anasema Mkenda.

Mapema mwezi uliopita, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Geofrey Mwambe, alipokuwa mkoani Tabora anakiri serikali kutambua upungufu, kwani mahitaji yaliyoko ni tani 564,000 kwa mwaka huku na uwezo ni 206,000, sawa na asilimia 36.5 .

Wakati wa kuzindua Kitabu cha Mwongozo wa Uwekezaji mkoani humo, Mwambe alisema Tabora ambayo ina uwezo wa kuzalisha mazao au mbegu za mafuta kama pamba na michikichi na fursa hiyo ikitumika vizuri itainua kiwango cha uchumi wake.

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Soma madarasa yote jirudie zako nyumbani






NA JOSEPH KULANGWA

HIVI karibuni nilikuwa mahali kijiweni na wenzangu, nikasikia malumbano fulani hivi ya hoja, yakitoka kwa marafiki zangu hao wakizungumzia elimu ya Tanzania na mustakabali wa maisha ya wasomi.

Ilianzia kwa mmoja ambaye alitoa takwimu alizokariri kutoka kwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, kwamba idadi ya wanafuzni wanaodahiliwa katika vyuo vikuu imeongezeka kutoka 65,064 mwaka 2015, hadi 87,813 mwaka jana.

Akasema takwimu hizo alizosoma kwenye moja ya magazeti makubwa nchini na akaziamini, akamkariri tena naibu waziri akisema lengo la serikali ni kuboresha elimu katika ngazi zote, kwa kuzingatia falsafa ya kujitegemea inayoendana na mazingira ya nchi.

Akabainisha zaidi, kuwa naibu waziri alikuwa akimaanisha mazingira ya nchi kuhusu elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi. Nikakumbuka kuwa hivi sasa huo ndio wimbo katika Taifa hili, kuboresha elimu kwa kufuata mazingira.

Ukiimbwa kuwa hivi sasa wanafunzi wa vyuo wasitarajie tu kuajiriwa bali wajiajiri. Kwamba wakishahitimu watafute cha kifanya, kwa sababu ajira serikalini hazipo na kama zipo, ni chache sana.

Wimbo huo nilishausikia sana na nikauelewa, kuwa kweli hali ndiyo hiyo, hivi sasa ukisoma ukamaliza chuo kikuu, ni bahati sana kupata ajira, vinginevyo ujiajiri. Lakini, utajiuliza ujiajiri wapi, je, ndicho kilichokuweka chuoni miaka mitatu, minne na mitano? Hapana! Inakuwaje sasa?

Katika kuchangia kwangu hapo kijiweni, nami nikasema nimekuwa nikisikia na kuona juhudi katika masuala ya ufundi, tena ambayo yamo katika ngazi za wanafunzi waliomaliza madarasa ya saba, 12 na pengine 14.

Sasa kama ndivyo inakuwaje mtu asome mpaka chuo kikuu na aishie mtaani, kwa sababu eti hakuna ajira? Tunajimwambafai vipi kuongeza idadi ya wadahiliwa, wakati wakimaliza vyuo wanarudi mitaani kuzurura?

Nami nikasema nishamsikia Jumanne Kishimba, mbunge wa Kahama, ambaye wala si msomi, lakini anachokisema, kinaashiria usomi asilia. Alihoji, inakuwaje uninyang'anye mwanangu mdogo ukakae naye miaka 20 na ushei, halafu unirudishie hawezi hata kulima wala kuchunga ng'ombe?

Mbaya zaidi unamkopesha ada asome chuo kikuu, ukitarajia kumdai atakapoanza kazi. Ataanza wapi na lini? Na lini atarejesha mkopo huo, kama hata hujui anafanya wapi kazi? Kwanini watoto hawa wasisome bure vyuoni ili warudi bure majumbani kwao?

Kishimba anasema, kwani kuna haja gani ya darasa kusomwa kwa mwaka mmoja! Anajua kuwa vichwa vya watu vinatofautiana, kuna wengine hata umuweke darasa moja miaka mitano, anaweza atoke kama alivyoingia, lakini wapo ambao anaweza kukaa darasani mitano tu, akawa kipanga.

Tunaendelea kuwa na mfumo wa elimu ileile ya miaka saba shule ya msingi, minne sekondari na miwili sekondari ya juu kabla ya mitatu, minne au mitano chuo kikuu, baada ya hapo, rudi nyumbani kaanze maisha ya kukaa upya na wazazi wako!

Hivi sasa tunahimiza vyuo vya ufundi, ambavyo ni vya kati, huku tukihitaji viongozi, lakini viongozi wanajengewa vyuo vya vyama, vyuo vya kiitikadi, humo ndimo tukitaka mkuu wa mkoa, mkuu wa wilaya, katibu tawala, mkurugenzi tunaangalia ukada wake tunampa kazi. Lakini tamko jipya, hata kada wa ng'ambo ya pili so habari anafikiwa rasmi katika uteule huo.

Huku kwingine, tukitaka kuajiri kwa nafasi kiduchu zilizopo, tunaangalia historia ya wazazi wa mwombaji, tunaangalia unasaba wake na mkuu wa kampuni au kiongozi wa kisiasa au kiserikali. Kama hatokani na hao, basi ajira ataisikia tu bombani.

Itakuja kufikia sasa wazazi kuona elimu ya chuo kikuu si malikitu, na ndiyo sababu polepole tunaanza kurejea kwenye falsafa ya Elimu ya Kujitegemea, ambayo tuliiua wenyewe. Tujiulize hivi kurejesha elimu hiyo enzi hizi za kidigitali, tutawapata wasomi kweli?

Hapa tunataka kuzungumzia masuala ya kujiajri katika kilimo kinachobatizwa jina la cha kisasa. Kilimo hicho kinaanzaje kwa mtoto aliyesoma nadharia ya mambo ya siasa, jamii au saikolojia chuo kikuu. Kwa mtaji upi lakini? Alamsiki!

BIASHARA

AGRI-CONNECT

# Mradi ulioibua mavuno mapya kahawa, maisha mapya walimaji Nyanda za Juu

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

KAHAWA imo katika mazao makuu ya biashara nchini, inayochangia kwa kiasi kikubwa mapato ya jumla kwa bidhaa zinazosafirishwa nje, ikiingiza fedha nyingi za kigeni kila mwaka.

Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB), inatoa pato la moja kwa moja kwa zaidi ya kaya za wakulima 400,000, ambayo ni wananchi milioni 2.4.

Mbeya ni mkoa unaolima kahawa na umekuwa wa kwanza kuzalisha aina ya Arabika, inayokadiriwa kuwa kati ya tani 12,000 hadi 15,000 kwa mwaka.

Hapo kuna Mradi wa Kuendeleza Kahawa katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, iki sehemu ya programu ijulikanayo kama Agri- Connect, mkakati wa pamoja kati ya Tanzania na Umoja wa Ulaya (EU).



Mkurugenzi Msaidizi wa Maendeleo ya Mazao kutoka Wizara ya Kilimo, Beatus Malema (aliyevaa suti nyeusi), akikabidhi kipima unyevu cha kahawa kwa mwanachama wa chama cha msingi cha mkoani Ruvuma, Christina Mbunda, katika kikao cha kuongezea mnyororo wa thamani zao hilo, kilichoandaliwa na shirika la Café Africa na wadau mbalimbali. **PICHA: GRACE MWAKALINGA.**

**DIRA YA PROGRAMU**

Ni programu inayolenga kuinua sekta kilimo katika Nyanda za Juu Kusini. Agri - Connect inayojumuisha kahawa, chai, matunda na mboga. Pia, inaboresha barabara kupitia Wakala wa Huduma za Barabara Vijijini na Mjini (TARURA)

Mradi wa Kuendeleza Kahawa -CODE P, Cafe Africa Tanzania, unatekelezwa kwa kushirikiana na Vi Agroforestry kutoka Mwanza kama shirika kiongozi (Lead Partiner), TaCRI, BRAC Maendeleo na ANSAF, wakifadhiliwa na EU.

Kwa Nyanda za Juu Kusini, lengo kuu ni kuchangia maendeleo ya zao hilo katika mnyororo wa thamani, kwa kuongezea wananchi kipato na kuboresha lishe kwa wakulima wadogo walima kahawa wa mikoa na wilaya zake katika mabano: Ruvuma (Mbinga na Nyasa), Mbeya (Mbeya Vijijini na Rungwe) na Songwe (Ileje na Mbozi).

Ni mikoa minne mradi imeiptia kuwalenga wakulima 24,000, kwa mgawayiko wanawake 14,400 na wanaume 9,600, walioko katika vyama vya Msingi vya Makulima (AMCOS) 60.

Utekelezaji mradi una dira, serikali ukinuia kuongeza tija ya kuzalisha kahawa. Cafe Africa Tanzania, imekabidhiwa jukumu la kuwasaidia wakulima na vyama vya msingi namna ya kusimamia mavuno na kuwajengea uwezo na mbinu za kuzingatia baada ya mavuno, maarufu 'post harvesting management' isipoteze ubora, uhifadhi salama na masoko.

**MENEJA MRADI**

Meneja Mradi wa Kahawa, Agri- Connect kwa mikoa Nyanda za Juu Kusini, Mbeya, Songwe na Ruvuma, Samora Mnyaonga, anasema matarajio yao ni kuviimarisha vyama 60 vya msingi na kuviwezesha kuwa vituo vya kutoa na kusambaza pembejeo za kilimo, teknolojia na maarifa.

Pia, ina mtazamo wa kuwezesha wataalamu wa kilimo bora cha kahawa kwa maofisa ugani serikalini na wadau wanaoshughulikia sera na mipango, wakiwapa mafunzo ya kilimo endelevu na matumizi bora ya ardhi.

Anasema mradi unaangalia kuwafikia na kuwawezesha wadau walioko katika mnyororo wa thamani wa kahawa, kufikia ufanisi kwenye uzalishaji.

"Kupitia mradi huu Cafe Africa, imekarabati miundombinu katika mitambo ya kuchakata kahawa yaani 'CPU' katika AMCOS 20 kwa mwaka huu wa kwanza wa utekelezaji wa mradi huu mbali na ukarabati huo mradi umewapatia vipima unyevu 20 katika AMCOS 20, ili kuthibiti kiwango cha unyevu wakati wa uanikaji wa kahawa," anasema Mnyaonga.

Anaongeza kuwa Cafe Africa Tanzania na TCB, waliandaa warsha kwa wadau kujadili masoko nchini na mnyororo wa kahawa, ikilenga kufungua uhusiano mzuri kwa wadau wanaojihusisha na kahawa, hasa wakulima, AMCOS, viwanda, wanunuzi na serikali.

**MAFANIKIO YAKE**

Mnyaonga anasema, katika mwaka fedha uliopo, Cafe Africa Tanzania, imetekeleza mradi huo katika mikoa yote mitatu na kuwafikia wakulima takriban 6,000, kati yao wanawake 4000 na wanaume 2000, katika AMCOS 39 kati ya 60 zilizopo.

Mkurugenzi wa Cafe Africa, Dafosa Sanga, anasema mradi unalenga kuongeza tija ya uzalishaji kahawa, kupitia ubora unaohitajika kukidhi viwango kwa soko la ndani na nje ya nchi.

Anataja mafanikio ya kuongezeka uzalishaji kwa kutumia mbinu bora za kilimo zinazohimili mabadiliko ya tabianchi, wakishirikiana na maofisa ugani wa maeneo.

Pia, anasema wamewafikia maofisa ugani 69 kutoka vijiji na kata zinazotekeleza mradi huo, mtazamo ni kuongeza kasi ya elimu na ushauri kitalaamu kwa wakulima, wazalishe kisasa na kuongezea familia kipato.

"Shilingi milioni 50 zimetumika kwa ajili ya kununua mashine za vipima unyevu 20 katika AMCOS 20, ili kudhibiti kiwango cha unyevu wakati wa uanikaji wa kahawa kwa ajili ya kuimarisha mazingira shindani ya biashara ya zao hilo, kutokana na sera na mifumo bora," anasema Sanga.

Anataja dira kuu ya mradi ni kupandisha pato la mkulima kwa kumpatia mbinu bora shambani baada ya kuongezea kahawa mnyororo wa thamani, kuanzia mchakato wa uvunaji, kuchakata na huduma jumuishi za fedha.

**MRADI SONGWE**

Meneja wa TaCRI, mkoani Songwe, Isaac Mushi, anasema wanaendeleza mikakati ya kuzalisha na kupanda miche ya kahawa, zitakazotumika katika shamba darasa kwa wakulima wahitaji.

Hapo anataja TaCRI ikishirikiana na TCB, wanazalisha miche mipya na kuwasambazia wakulima, kuwashauri kitalaamu kuhusu mbegu sahihi kwa eneo husika, ili kumsaidia mkulima avune zaidi.

Mushi pia anataja tija, ubora na ushindani wa kahawa kwenye soko la dunia, kipato kwa mkulima na pato la taifa, mafanikio yake yanategemea ubora wa miundombinu na matumizi sahihi ya viuatilifu.

Anahimiza ubora wa kahawa unamhiaji mkulima kuzingatia kanuni anazozitaja ziko kuongeza ubora wa kahawa na wao wanahamasisha wakulima kukoboa kahawa kijijini au katika kaya.

**KUTOKA WIZARANI**

Mkurugenzi Msaidizi Maendeleo ya mazao kutoka Wizara ya Kilimo, Beatus Malema, anataja vikwazo wanavyokutana navyo wakulima, ni baadhi ya warajisi wa vyama vya ushirika wanashindwa kusimamia na kuwawajibisha viongozi wa vyama hivyo, wanatumia vibaya fedha za umma.

Anakiri wizara inapokea malalamiko ya tuhuma za wizi wa fedha za ushirika kila mara, hivyo anawaonya warajisi wawe makini na kuwawajibisha wafujaji wa mali za ushirika, akionya atakayeshindwa kutimiza majukumu, atashughulikiwa kisheria.

Malema anaeleza mikakati ya serikali, ni kuhakikisha kahawa inakuwa mkombozi wa mkulima, kwa kuhakikisha pembejeo za kilimo zinapatikana kupitia vyama vya ushirika, hali anayoamini itadhibiti uchakachuaji unaofanywa na baadhi ya watu, wengine wakiwauzia kwa bei kubwa.

**BOSI TCB**

Kajivu Kisenge kutoka TCB, anasema Tanzania inakabiliwa na kikwazo cha kuporomoka bei ya zao hilo katika soko la ndani na kimataifa.

Anasema hivi sasa wanabuni mbinu bora za kupanga gharama za usafirishaji, vifungashio na kodi za nishati, sambamba na kuzingatiaji kanuni zilizorekebishwa, ili kuboresha ushindani wa bei shambani na mnadani, kuvutia wateja wengi zaidi.

Mkulima wa kahawa, Penson Nkoswe, anayemiliki kiwanda cha kukoboa Kahawa wilayani Mbozi, anaunga mkono ukweli wa tatizo bei ya kahawa kushuka kiholela.





# Kiini uhaba mafuta hadharani

Na Renatha Msungu, DODOMA

SERIKALI imesema viwanda vya mafuta ya kula vinalazimika kuzalisha kwa miezi sita badala ya mwaka mzima kutokana na uhaba wa mbegu za mafuta ya alizeti uliopo nchini.

Imesema hatua mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa katika kukabiliana na hali hiyo ikiwamo kutambulisha mbegu mpya ya alizeti aina ya Records inayozalishwa na Wakala wa Mbegu (ASA) ambayo imeonyesha kuwa na matokeo mazuri kwa wakulima.

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, aliyasema hayo juzi alipokagua kiwanda cha kuzalisha mafuta ya alizeti cha Pyxus kilichopo jijini hapa.

Bashe alisema Tanzania inakabiliwa na upungufu wa tani 400,000 za mafuta ya kula.

"Tunahitaji tupate mbegu bora ili tuweze kukidhi mahitaji hayo, tumekuwa tukitumia fedha nyingi kuagiza mafuta," alisema.

Naibu waziri huyo alisema zingekuwapo mbegu bora, uzalishaji wa mafuta ungekuwa wa kutosha na kuiepusha serikali kuagiza mafuta ya kula nje ya nchi.

"Serikali tumeamua kushirikiana na viwanda kwa ajili ya kutafuta mbegu bora za mafuta ya alizeti, tutawatumia wakala wa mbegu nchini (ASA) lakini pia tutaingalia mbegu ya Records ambayo wakulima wanasema inaonyesha kuwa na matokeo mazuri," alisema Bashe.

Alisema kiuhalisia kiwanda hicho kinahitaji tani 20,000 lakini kwa sasa wanapata tani 10,000 ambazo hazitoshelezi na kuongeza kuwa endapo wangepata kiasi halisi wanachohitaji, ingesaidia kutatua tatizo la mafuta.

Alisema anaamini serikali kwa kushirikiana na wadau wa uzalishaji mafuta nchini watatatua tatizo la uzalishaji wa mafuta ya kula nchini.

"Mahitaji ya mbegu za kuingia viwandani ni zaidi ya tani milioni 1.3 ili kuzalisha mafuta ya kula," alisema.

Aliongeza kuwa wameipa kipaumbele mikoa ya Dodoma, Singida na Simiyu katika uzalishaji wa mafuta ya alizeti wakati wakiendelea kuangalia mikoa mingine ili kutengeneza mfumo wa uwezeshaji ambao wizara itashirikiana na wanunuzi na wasambazaji wa mbegu. Alisema serikali haiwezi kumzuia mtu kuuza mafuta endapo tu anafuata taratibu na sheria za uuzaji bidhaa hizo.

Bashe aliwataka wawekezaji kutojifungia peke yao pale wanapokumbana na vikwazo mbalimbali katika uendeshaji wa shughuli zao.

Mkugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha Pyxus, Malcom Mcgrath, alisema wazalishaji wapo tayari kushirikiana na serikali kuhakikisha wanatatua kero ya mafuta ya kula nchini.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha Pyxus, Malcom McGrath (kulia), akitoa maelezo kwa Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (wa pili kulia), kuhusu uzalishaji wa mafuta ya alizeti unaofanywa kiwandani hapo, jijini Dodoma juzi.
PICHA: RENATHA MSUNGU

# Uvunaji mkurungu waruhusiwa

Na Ibrahm Joseph, DODOMA

WIZARA ya Maliasili na Utalii imeondoa zuio la uvunaji na biashara ya usafirishaji wa miti jamii ya mkurungu ambayo ilizuiwa kwa zaidi ya miaka mitatu.

Naibu Waziri, Mary Masanja, aliyasema hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Masanja alisema serikali imeondoa zuio hilo ambalo lilitolewa tangu mwaka 2018.

"Kwa taarifa hii ninapenda kusema kuwa serikali imeridhia shughuli za uvunaji na usafirishaji wa mazao yatokanayo na mti aina ya mkurungu kufanyika ndani na nje ya nchi kwa mujibu wa sheria," alisema.

Naibu waziri huyo alisema kuondolewa kwa zuio hilo kunatokana na kukamilika kwa tathimini iliyokuwa ikiendelea kuhusu miti hiyo na serikali imejiridhisha imeongezeka na hivyo unavunaji kuruhusiwa.

Aliyataja maeneo ambayo miti hiyo itaanza kuvunwa kuwa ni mikoa ya kanda ya magharibi ambayo ni Tabora, Kigoma, Katavi, Mbeya na Rukwa.

Mary alisema miti hiyo pia inapatikana kwenye nchi jirani za Zambia, Msumbiji na Kongo DR.

Alibanisha soko la ndani la mti huu ni dogo na faida yake bado ipo chini kwa pande zote yaani serikali na wafanyabiashara.

Alisema katika kipindi cha mwezi moja kuanzia Juni 2 hadi Julai 2 mwaka huu, wale wote wenye mzigo uliopatikana kwa njia halali na wanahitaji kupata vibali vya kusafirisha nje mazao ya mti huo, watapewa vibali hivyo na Waziri wa Maliasili na Utalii.

Masanja aliongeza kuwa wale wote wenye nia ya kuendelea na uvunaji na biashara ya mti huo, watapaswa kuomba vibali vya uvunaji kwa mujibu wa mwongozo wa uvunaji kwa mwaka wa fedha wa 2021/22.

Aliyataja baadhi ya masharti wanayotakiwa kufuata wafanyabiashara kuwa ni kuomba vibali vya uvunaji kupitia kamati za uvunaji za wilaya ambazo mwenyekiti wake ni mkuu wa wilaya husika.

Masharti mengine ni kuvuna kwa kuzingatia leseni zitakazotolewa kwa maeneo husika na kujiepusha na ununuzi wa mizigo toka kwa watu ambao hawajaidhinishwa.

Pia, alisema watumishi na wafanyabiashara wote watakaohusika katika uvunaji, usafirishaji na biashara wa mti huo watatakiwa kutambulika na mamlaka husika na kuwaonya wananchi kujiepusha na vitendo vya biashara haramu.

# Chuo chajipanga utafiti wa kitaifa

Na Augusta Njoji, DODOMA

CHUO cha Mipango na Maendeleo ya Vijijini (IRDP), kimesema kitaendelea kufanya utafiti mbalimbali ili kusaidia serikali kwenye mipango yake ya kutatua kero zinazoikabili jamii.

Mratibu Msaidizi wa Miradi ya Maendeleo Vijijini na Mhadhiri wa chuo hicho, Christopher Mdoe, aliyasema hayo juzi kwenye maonyesho ya vyuo vya elimu ya ufundi yaliyofanyika jijini hapa.

Alisema chuo hicho kina kazi kubwa tatu za kufanya utafiti, kufundisha na kuzalisha na kutoa ushauri na uelekeze kwenye mambo yanayohusu mipango ya maendeleo.

"Utafiti unafanywa na wahadhiri na wanafunzi, huwezi kuhitimu Chuo cha Mipango bila kufanya utafiti na kuleta matokeo katika kubadilisha hali fulani maana utafiti ni kutafuta suluhisho kwa changamoto ambayo imeibuka," alisema.

Mdoe alisema kuna utafiti ulifanywa na chuo hicho katika mikoa ya kanda ya ziwa ambao uliangalia kiwango cha umaskini na kubaini kuna umaskini kwa sababu kilimo kinachofanyika siyo rafiki kutokana na mabadiliko ya tabia nchi.

Alibainisha kuwa kupitia utafiti huo, wamebuni miradi ya kuwasaidia wananchi ikiwamo kilimo cha viazi lishe ambapo kuna viwanda vimeanzishwa na chuo hicho kwa ajili ya kusaga unga wa viazi na kuuza.

"Unga huu pia unatumika kwa uji lakini kuzalisha biskuti ambapo kuna watu wanatoka Nairobi na Dar es Salaam kununua kutoka kwa mkulima, chuo kimewezesha wakulima kule vijijini kwenye suala la afya na kipato.

"Kwa siku hizi saba tumetoa elimu kwa wananchi kuhusu miradi na utafiti unaofanya ambao una tija kwa wakulima na wafugaji, tuna kozi mbalimbali za kuzalisha wataalamu na katika kulelekea uchumi wa viwanda Chuo cha Mipango kinafanya kazi kubwa kwa kuwa tunazalisha wataalamu ambao wanakwenda kufanya kazi kwenye viwanda hivyo," alisema.

Mhadhiri huyo alisema hata katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa, chuo hicho kimeshiriki kuandika na kitahakikisha kinazalisha wataalamu wenye ujuzi utakaosaidia taifa kufikia azma yake ya kujenga uchumi wa viwanda.

**"Unga huu pia unatumika kwa uji lakini kuzalisha biskuti ambapo kuna watu wanatoka Nairobi na Dar es Salaam kununua kutoka kwa mkulima, chuo kimewezesha wakulima kule vijijini kwenye suala la afya na kipato.**



## Wakulima watakiwa kujiunga AMCOS

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

SERIKALI wilayani Rungwe katika Mkoa wa Mbeya, imewataka wakulima na wafugaji kujiunga kwenye vyama vya ushirika (AMCOS) ili iwe rahisi kunufaika na huduma mbalimbali zinazotolewa na serikali pamoja na taasisi mbalimbali.

Mkuu wa wilaya hiyo, Juius Chalya, alitoa agizo hilo juzi wakati wa kutiliana saini hati ya makubaliano ya kuwakopesha wafugaji hao fedha kwa ajili ya bima ya afya baina ya Chama cha Wafugaji na watendaji wa Benki ya CRDB na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).

Alisema serikali ama taasisi mbalimbali zinazowahudumia wananchi hazitoi huduma kwa mwananchi mmoja mmoja na badala yake zinatoa kwenye vikundi vikiwemo vyama vya ushirika.

"Hawa watu wa Benki ya CRDB na Mfuko wa Bima ya Afya, wamekuja kutoa huduma hii kwa sababu wanajua kwamba ninyi wazalishaji wa maziwa mmeunganishwa kwenye umoja wenu, sasa maelekezo ya serikali ni wazalishaji wote kuungana kwenye vyama vya ushirika," alisema Chalya.

Alisema wilaya hiyo ina wazalishaji wa mazao mbalimbali yakiwamo ndizi, viazi, chai na maparachichi ambayo kwa sasa yana soko kubwa duniani.

Mkuu wa Biashara wa Benki ya CRDB kutoka Makao Makuu, Joseph Witts, alisema makubaliano hayo yatasaidia pia kuongeza mnyororo wa thamani wa mazao ya wakulima kwa kuwa kila mmoja atawajibika vizuri kwenye eneo lake.

Alisema wakulima watazalisha vizuri, Benki ya CRDB itatoa mikopo kwa wakulima ili kuendeleza shughuli zao na NHIF watahakikisha wakulima wanakuwa na uhakika wa matibabu.

"Haya ni makubaliano muhimu sana na yatawasaidia sana wakulima, sisi tutawahakikishia wakulima wa nchi hii huduma bora za afya ili wazalishe kwa tija," alisema Witts.

Mkurugenzi wa huduma za wanachama wa NHIF kutoka makao makuu ya mfuko huo, Christopher Mapunda, alisema lengo la makubaliano hayo ni kuongeza wigo wa wananchi wanaonufaika na Bima ya afya ikiwa ni utekelezaji wa nia ya Serikali ya kila Mtanzania kuwa na bima.

Alisema kwa sasa idadi ya Watanzania wanaotumia bima ya afya ni ndogo hali ambayo inalifanya kundi kubwa la wananchi kuwa nje ya mfumo na kupata shida wakati wa kutafuta huduma za matibabu hasa wakulima ambao wengi hutegemea kupata fedha wakati wa mavuno.

# MV Mbeya yaponza maofisa wawili TPA

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, ameagiza maofisa wawili wa Mamlaka ya Bandari nchini (TPA) waondolewe kwenye nyadhifa zao kwa tuhuma za kushindwa kufanyia kazi taarifa zilizohatarisha usalama wa meli ya abiria ya MV Mbeya II iliyonusurika kuzama hivi karibuni baada ya kupigwa na dhoruba.

Waitara aliwataja maofisa hao kuwa ni Kaimu Meneja Mkuu wa Bandari za Ziwa Nyasa, Mhandisi Hamis Nyembo na Kapteni Abdallah Mwengamno, Makao Makuu ya Mamlaka ya Bandari (TPA), akitaka wapangiwe kazi zingine.

Alitoa agizo hilo juzi baada ya kufanya kikao na wadau wa meli za Ziwa Nyasa na kubaini kuwa maofisa hao walishapewa taarifa za kuwapo kwa hitilafu kwenye meli ya MV Mbeya II muda mrefu, lakini hawakuchukua hatua zozote ili hitilafu hizo zifanyiwe kazi.

"Manahodha wa meli hizo baada ya kusafiri meli hii kwenda Ruvuma, waliporudi walitoa taarifa kwa maandishi na kumkabidhi huyu Injinia Nyembo, ambaye pia alizifikisha taarifa hizo kwa Kapteni Mwengano aliye makao makuu ya TPA, lakini hakuna hatua walizochukua na wakaruhusu chombo hiki kuendelea kufanya kazi," alisema Waitara na kuongeza.

"Hivyo naagiza hawa waondolewe kwenye nafasi zao ili waje watu wengine tufanye kazi, serikali inachotaka sasa hivi ni watu wanaofanya kazi na kuonyesha matokeo na ndio maana rais alibadilisha Mkurugenzi Mkuu wa TPA," aliongeza.

Kadhalika, Waitara alitoa siku 14 kwa uongozi wa TPA kushirikiana na mtengenezaji wa meli hiyo Kampuni ya Songoro Marine, kuhakikisha hitilafu zilizo kwenye Meli ya MV Mbeya II na meli zingine zilizojengwa na kampuni hiyo zinarekebishwa ili huduma zirejee na kabla hazijaanza kufaya kazi lazima wasaini makubaliano maalumu.

Pia, alitoa siku 14 kwa TPA kushughulikia madai ya wafanyakazi wa Bandari za Ziwa Nyasa ili wafanyakazi wafanye kazi kwa moyo kwa maelezo kuwa lengo la serikali ni kuhakikisha TPA inafika muda ambao itajiendesha kwa faida.

Aliagiza watendaji wa Wakala Huduma za Meli nchini (TASAC), kuzifanyia tathmini meli zote za abiria zinazofanya kazi ndani ya Ziwa Nyasa na kutolea taarifa ili kama kuna matatizo yarekebishwe.

Akizungumzia tatizo lililoikumba meli ya MV Mbeya II, Mkurugenzi Mtendaji wa TASAC, Kaimu Mkeyenge, alisema baada ya meli hiyo kupigwa na dhoruba waliifanyia uchunguzi na kubaini ilipata madhara kwenye maeneo mbalimbali.

Alisema walibaini kuwa maji yaliingia kwenye mfumo wa injini na kusababisha hitilafu upande wa kulia ya meli hiyo na kwamba mawimbi yalikuwa sio ya kawaida na ndio maana maji yaliingia kwenye eneo ambalo huwa sio kawaida kufika.

Pia, taa upande wa kulia ziliharibika na hivyo kuwa vigumu meli hiyo kuonekana usiku na tatizo hilo lilisababisha ugumu hata wakati wa uokozi.

"Kwa sasa tunaahidi kufanyia kazi maagizo ya Naibu waziri ili kuhakikisha kwamba watumiaji wa vyombo hivi wanakuwa salama wakati wote, lakini tulishafanya tathimini kabla Meli haijaanza kufanya kazi na hata baada ya kuanza kazi kulikuwa hakuna tatizo ila kilichotokea ni matukio ya asili," alisema Mkeyenge.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa TPA, Erick Hamis, alisema watahakikisha wanafanyia kazi maelekezo yote ya Naibu waziri ili meli hizo zinakuwa na usalama wa kutosha kwa abiria na mizigo.

Alisema TPA ni chombo cha biashara na kitendo cha meli hiyo kusimama kufanya kazi ni hasara kubwa kwa Mamlaka.

Mbunge wa Jimbo la Kyela, Ally Jumbe, aliomba wananchi wa Wilaya ya Kyela wawe wanapatiwa taarifa sahihi za usafiri huo.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (kulia), akisikiliza maelezo ya moja ya taasisi zilizohudhuria kwenye maonyesho ya Siku ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HELSB), katika Chuo Kikuu cha Mzumbe Kampasi ya Mbeya hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Shule yakabiliwa upungufu matundu ya choo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SHULE YA Sekondari Mponja iliyopo jijini Mbeya inakabiliwa na upungufu wa matundu 12 kwa ajili ya wasichana hali ambayo inawalazimu kuhatarisha maisha yao kwa kutumia vyoo vichache vilivyopo.

Hayo yalisemwa jana na Mkamu Mkuu wa shule hiyo, Festus Sawalla, wakati Mbunge wa Viti maalumu wa Mkoa wa Mbeya, Maryprisca Mahundi kwa kushirikiana na madiwani wa Viti maalumu wa Jiji la Mbeya, walipokuwa wanakabidhi msaada wa mifuko 10 ya saruji kwa ajili ya ujenzi wa vyoo. Alisema tatizo la upungufu wa vyoo shuleni hapo lilikuwa la muda mrefu na wanafunzi walikuwa wanapata shida kubwa hasa watoto wa kike ambao huwa wanahitaji huduma maalumu wanapokuwa kwenye siku za hedhi.

"Tunawashukuru sana madiwani wetu na mheshimiwa mbunge kwa kuliona tatizo hili na kutusaidia mifuko hii, tunaamini itatusaidia sana kukamilisha vyoo hivi na watoto wetu waendelee kuvitumia na kulinda afya zao," alisema Sawalla.

Aliwaomba wadau wengine waendelee kuisaidia shule hiyo kwa maelezo kuwa bado hawajafikia lengo la kukamilisha vyoo hivyo ili vianze kutumika.

Mbunge wa Viti Maalumu, Mahundi ambaye pia ni Naibu waziri wa Maji, alisema aliamua kushirikiana na wananchi kujenga vyoo hivyo ili kupunguza tatizo hilo.

Aliomba wananchi waendelee kujitolea kwenye shughuli za maendeleo katika kipindi hiki ambacho serikali inatekeleza sera ya elimu bila malipo.

"Tunaomba pia halmashauri ijitahidi kuchangia pia hasa kumalizia hiki choo, kwa hapa ujenzi ulipofikia imebakia ni kuezeka tu na kumalizia ndani ili kianze kutumiwa na mabinti zetu waanze kukitumia," alisema Mahundi.

Kwa upande wake Diwani wa Kata ya Igawilo, Anna Ndindi, alisema madiwani wanawake waliguswa na uhaba huo kwa ajili ya wasichana na ndio maana waliamua kuchangishana ili kupata mifuko hiyo.

Alisema watoto wa kike ndio wenye hatari zaidi ya kupata maradhi kwa kutumia vyoo vichafu kuliko ilivyo kwa wavulana na kwamba baadhi ya magonjwa ambayo huwa yanawasumbua wasichana ni maambukizi kwenye njia ya mkojo.

Alisema wataendelea kuchangishana ili wasaidie kuboresha miundombinu ya shule zingine za jiji hilo ili kuhakikisha wanafunzi wanajisaidia kwenye mazingira safi.



# Matatani tuhuma kusafirisha baiskeli, sukari ya magendo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KIKOSI Maalum cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM), kimewakamata watu watano kwa tuhuma za kusafirisha kwa magendo viroba 140 vya sukari vya kilo 50, runinga bapa tisa za nchi 50 na baiskeli tisa.

Kaimu Mkuu wa Kamandi ya Kusini ya KMKM, Luteni Kamanda Hassan Hussein Ali, alisema askari wao wakiwa doria za kawaida, waliwakamata watu hao katika maeneo ya Bahari ya Mason na Pungume Mkoa wa Kusini Unguja mnamo majira ya saa 7:30 usiku wa kuamkia jana wakielekea Dar es Salaam na mzigo huo.

Aliwataja watuhumiwa kuwa ni Zamir Khamis Ronga (30) ambaye nahodha wa jahazi, Yussuf Twaha Yussuf (36), Khamis Mohammed (45), Abdulwahid Abdulwarith Abdulwahid (35) na Abdu Ali Omar, wote wakazi wa Kisiwa Cha Uzi Mkoa wa Kusini Unguja.

Kaimu Mkuu huyo aliwataka wananchi kuacha tabia za kusafirisha bidhaa kinyume cha sheria kufanya kwa kuwa wanasababisha serikali kukosa mapato.

Alisema mbali na serikali kuikosesha mapato, pia wenyewe hupoteza au kuua mitaji ya biashara zao pindi wanapokamatwa, hivyo ni vyema kufuata sheria bila ya kushurutishwa.

Mkuu wa Wilaya ya Kusini, Rashid Makame Shamsi, alikipongeza Kikosi cha KMKM kwa kazi nzuri kinazofanya za kuisaidia serikali isipoteze mapato yake.

Alihimiza ushirikiano katika taasisi zingine za ulinzi na usalama ili kuziba mianya ambayo inaweza kutumiwa na wahujumu uchumi kwa maslahi yao.

Akizungumzia ucheleweshwaji wa kesi za biashara za magendo, mkuu huyo wa wilaya alimtaka Kaimu Mkuu wa Kamandi wa KMKM kufanyia kazi na kumwahidi kuwa ataziwasilisha kwake kesi zote zilizokuwa hazijapatiwa ufumbuzi wilaya mwake.

Ofisa Uhusiano ZRB, Makame Khamis Mohammed, alisema kuchukua mzigo wowote bila ya vibali maalum ambavyo vinaonyesha uhalali na malipo ya mzigo huo ni kosa kisheria na mtu yeyote anayefanya hivyo anastahiki kushtakiwa kwa kosa la kuikosesha mapato serikali.

Ofisa huyo aliwataka wananchi kufuata sheria na kusafirisha mizigo yao katika bandari ili kuepuka usumbufu.



Mkuu wa Wilaya ya Kusini Unguja, Rashid Makame Shamsi (wapili kushoto), akizungumza na wakuu wa Kikosi cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM), baada ya kikosi hicho kukamata viroba 50 vya sukari vilivyokua vikisafirishwa kinyume na sheria kutoka Zanzibar kwenda Dar es Salaam kupitia bandari bubu jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Sakho atoa darasa malezi ya watoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MCHEZAJI wa timu ya soka ya Crystal Palace ya Uingereza na timu ya taifa ya Ufaransa, Mamadou Sakho, imetaka jamii kushirikiana katika malezi ya watoto.

Amesema ukatili wa kijinsia umekuwa kikwazo kikubwa kwa watoto kupata maendeleo ya ukuaji na kutimiza ndoto zao za maisha.

Sakho alitoa rai hiyo juzi alipozuru katika kijiji cha kulelea watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu cha SOS Zanzibar wakati wa ziara yake ya kuunga mkono maendeleo ya watoto na kutangaza sekta ya utalii Zanzibar.

Alisema chanzo cha watoto wa mitaani ni matokeo ya jamii kukosa ushirikiano katika malezi ya watoto kufuatia watoto hao kupoteza wazazi wao kwa njia mbalimbali.

Sakho alisema ukatili wanaofanyiwa watoto ni kikwazo kikubwa kinachozikabili nchi nyingi duniani ikiwamo Bara la Afrika, hatua ambayo huibua watoto wa mitaani na kukabiliwa na ukatili wa aina mbalimbali.

"Watoto lazima wawe huru na aina zote za ukatili ambazo zimekuwa zikirudisha nyuma kutimiza ndoto zao na makuzi na maendeleo ikiwamo elimu," alisema.

Alikipongeza kituo cha SOS Zanzibar katika juhudi za kuwatunza watoto na kuwapatia huduma zote zinazostahiki kwa mujibu wa sheria na haki za watoto.

Mkurugenzi wa SOS Zanzibar, Asha Salim, alimtaka mchezaji huyo kuwa balozi mzuri katika kuhakikisha watoto wanaishi salama na kuepukana na aina zote za udhalilishaji na ukatili.

Alisema watoto wengi bado hawapo salama na wanakabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwamo ukatili na ubakaji ambao huwaathiri kisaikolojia kwa muda wote wa maisha yao, hasa walioopoteza wazazi wao.

Alibainisha kuwa Kijiji cha SOS chenye jumla ya watoto 189 na wengine 2,000 ambao wanaishi nje ya kijiji hicho, kinaendelea na majukumu yake ya kuwapatia matunzo watoto ambao wamepoteza walezi kutoka kwa wazazi wao kwa njia tofauti.

"Kijiji cha SOS kinakuomba uwe balozi mzuri kwa ajili ya kupambana na ukatili wa kijinsia unaotokana na watoto kukosa malezi bora kutoka katika familia zao na kuona haki za watoto zinatimizwa kwa mujibu wa mikataba ya kimataifa," alisema.

Akiwasilisha salamu kwa niaba ya watoto wa Kijiji cha SOS Zanzibar, mtoto Hamida Shaaban, alimpongeza mchezaji huyo kwa ziara yake ambayo lengo lake ni kutangaza vijiji vya aina hiyo.

Sakho alikuwapo Zanzibar kwa ajili ya ziara ya kuitangaza katika sekta ya utalii, alikutana na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, Ikulu.

# SMZ yapata jibu uhaba wa maji

**Na Mwandishi Wetu** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imesema utekelezaji wa miradi miwili ya upatikanaji wa maji safi na salama unaotekelezwa na serikali ya India kupitia Benki ya Exim utasaidia kutatua tatizo la uhaba wa maji Zanzibar.

Waziri wa Maji, Nishati na Madini, Suleiman Masoud Mohamed, aliyesema hayo jana alipojibu hoja za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliokuwa wakijadili makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/22 Chukwani, Zanzibar.

Alisema mradi wa uhuishaji na uimarishaji wa miundombinu ya maji ambao utagharimu Dola za Marekani milioni 92.18 na mradi wa maji safi na mazingira utakaogharimu Dola milioni 35, itasaidia kwa kiasi kikubwa na kuwawezesha wakazi wa Mkoa wa Magharibi kupata maji safi na salama.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatekeleza miradi miwili inayogharamiwa na Benki ya Exim kutoka India ambayo ni muhimu na itasaidia upatikanaji wa maji safi na salama katika Mkoa wa Magharibi Unguja," alisema.

Waziri huyo alisema kazi kubwa inayofanywa na Mamlaka ya Maji Safi na Salama (ZAWA) kwa sasa ni kulinda miundombinu ya maji safi na salama pamoja na kujenga vyanzo hivyo kwa kuzungushiwa uzio.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano kumejitokeza tatizo kubwa la wananchi kuvamia vyanzo vya maji na kujenga makazi ya kudumu.

"Tunakabiliwa na tatizo moja kubwa la uvamizi wa vyanzo vya maji safi na salama ambapo sasa visima vyote vya mamlaka ya maji safi na salama vitajengewa uzio," alisema.

Waziri huyo alisema kazi inaendelea na utekelezaji wa mradi wa kuchimba visima wa Ras Al Khaimah ambao ni ujenzi wa visima na kuweka miundombinu ya usambazaji maji safi na salama katika mikoa ya Unguja na Pemba.

Alisema zaidi ya visima 30 vipo katika hatua ya mwisho ya kuwekewa umeme kwa ajili ya kuanza uzalishaji na kusambaza huduma hizo kwa wananchi.

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliidhinisha jumla ya Sh. bilioni 98.635 kwa ajili ya matumizi ya wizara hiyo katika mwaka ujao wa fedha.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**Uza,**
**Chenye Thamani Kubwa**
**Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0782253676**

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**EDEN RODRICK MASHAYO** anatangaza kupotelewa na Hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE 269963** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe **03/01/2020.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **GBD/RB/53/021.**

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI NA 52 YA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**BETHUEL MPAKANI KASEFU MMILLA**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**FLORA BETHUEL MMILLA**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji/mwombaji hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 28 mwezi wa 06 2021
Imewasilishwa Dar Es Salaam leo tarehe 31 mwezi wa 05 2021.

HAIDU MSAJILI

---

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.
KUITWA SHAURINI
KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MASWA
SHAURI NAMBA 26 YA MWAKA 2021.

KESI YA MADAI YA ARDHI KATI YA MAPULISHI HIMA (MWOMBAJI) DHIDI YA ESTER MADATA (MJIBU MAOMBI)

Ester Madata unatakiwa kuhudhuria katika baraza la ardhi na nyumba la wilaya ya Maswa kwenye shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 24/6/2021 saa 02.30 asubuhi.
Unajulisha kwamba iwapo utakaidi kupokea wito huu au kupuuza bila udhuru na kushindwa kufika siku iliyopangwa ,Baraza litalazimika kusikiliza maombi hata upande mmoja na kutoa uamuzi dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa amri ya mwenyekiti wa Baraza la ardhi na nyumba la wilaya ya Maswa leo tarehe 24 mwezi wa tano mwaka 2021.

J.T.KAARE
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MASWA.

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MARIAM BENARD MASSAWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **NISAN XTRAIL** yenye namba za usajili **T 449 BQZ** Chassis **No. NT30049637**, Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/DOM/R-B/271277/2021.**

---

**Summons to appear (O.VR.20 (1) of (CPC)**
**(Substituted Service)**
**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**
**MISC.LAND APPLICATION NO 679 of 2020**
**ROSEMARY CHIZA MALINZI……………………….APPLICATION**
**VERSUS**
**CARGO STAR LTD & 3 OTHERS…………………. RESPONDENTS**

**TO: 1. CARGO STAR LTD,**
**2. DIONIZ MALINZI,**

**WHEREAS:** The above named **APPLICANT** has institute the **APPLICATION** against you, you are hereby summoned to appear in this court in person or by advocate or authorized Agent on **28TH day of JULY,** 2021 at 09:00AM Before Hon. S. **KALUNDE JUDGE,** in the morning to answer the said **APPLICANT**, and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your **REPLAY.**

**TAKE NOTICE** that, in default of your appearance on that day the **APPLICATION** will be heard and determined in your absence.
Given under my hand the seal of this court, this **26TH day of MAY, 2021.**

DEPUTY REGISTRAR

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MECKSON RAPHAEL** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T.665 DQD** aina ya **HORSG**, yenye Tela no. **T.871 DQM.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya polisi: **KAH/RB/TR/232/2021.**

---

## TUNAPANGISHA

PR STADIUM HOTEL ILIYOPO KARIBU NA UWANJA WA TAIFA TEMEKE TUNA-PANGISHA "BAR" NA "LOUNGE" KWA BEI NAFUU SANA. KWA MAWASILIANO PIGA SIMU NO: 0764 822 509 / 0762 215 470.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZO KARIAKOO**
**POPOTE ULIPO**

**Ndugu, ROBERTSON MICHAEL SIMBAGIJE**

**WITO KUITWA SHAURINI**
**KESI YA MADAI 96/2021 NA…..**
**MDAI EDWARD EPIMARK LASWAI**
**MDAIWA ROBERTSON MICHAEL SIMBAGIJE**

Unaamriwa na mahakama ya mwanzo kariakoo kuja kusikiliza shauri la madai ya PESA Na 96/2021 siku ya JUMANNE tarehe 15/6/2021 saa 2:30 asubuhi,kama hukudhuria shauri litasikilizwa upande mmoja.

Amri hii imetolewa leo tarehe **02-06-2021.**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
KARIAKOO

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HILLARY REVOCATUS LYABANDI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA SIENTA** yenye namba za usajili **T 965 DRX** chasisi namba **NCP810071845** engine namba **1NZB386530,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **CONTROL NAMBA 9910823364099**

---

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**(JUDICIARY)**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA MOROGORO**

**MKOA MOROGORO**

**YAH: SHAURI LA MAREJEO (REVISION) NAMBA 01/2021**

**JOANITHA EHUDI MPOLELA………MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**BAKARY HAMISI……….MJIBU MAOMBI WA KWANZA**

**JUMA ISMAIL …………...MJIBU MAOMBI WA PILI**

MDAIWA WA PILI JUMA ISMAIL ANATAKIWA KUHUDHURIA MAHAKAMANI TAREHE 16/06/2021 SAA 2:30 ASUBUHI BILA KUKOSA

KUSHINDWA KUFANYA HIVYO KESI ITASIKILIZ-WA UPANDE MMOJA BILA KUWEPO

M.R. HAMDUNI
HAKIMU MKAZI MWANDAMIZI (W)
MOROGORO

---

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**Mikocheni Industial Area,**
**Po.Box 31042, Dar es Salaam.**
**Mob: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Wachache washiriki Siku ya Mashahidi Uganda

**Kampala,** UGANDA

MAADHIMISHO ya siku ya Mashahidi wa Uganda yamefanyika katika eneo la Namugongo, huku ikihudhuriwa na watu wachache ikilinganishwa na miaka iliyopita.

Huu ni mwaka wa pili bila waumini wengi kuwakumbuka mashahidi wa Namugongo, waliouawa na Mfalme wa Buganda, kwa Imani zao za kidini kutokana na janga la Covid-19.

Mwaka jana, hapakuwa na waumini wowote katika eneo hilo la Namugongo, kutokana na janga la corona, ingawa mwaka huu, walau wameruhusiwa watu wasiozidi 200, katika eneo hilo ambalo kwa kawaida huwapokea zaidi ya watu milioni mbili.

Ibada ya kuwakumbuka mashahidi wa Uganda, hufanyika kila mwaka, Namugongo, kuwakumbuka waumini wa kikristo 45, Waanglikana 33 na Wakatoliki 22, waliouawa kwa kukaidi amri ya Mfame wa Buganda, ambaye aliwataka wazikane imani ya dini yao.

Kabla ya kutokea kwa janga la virusi vya corona, mamilioni ya watu walifurika kutoka kila kona ya dunia katika eneo hilo, kuhudhuria maadhimisho hayo muhimu katika dini za Kianglikana na Kikatoliki.

Baadhi ya watu kutoka Uganda na nchi jirani, walitembea kwa miguu umbali mrefu kuhudhuria ibada Namugongo, alisema Padri Vincet Lubega, kutoka Jimbo katoliki la Masaka.

Sister Rose Gisare aliiambia BBC kuwa, walishiriki ibada licha ya changamoto ya janga la Covid-19.

Kila mwaka Juni 3, eneo la kilima la Namugongo, hushamiri pia kwa biashara mbalimbali, wageni kutoka maeneo tofauti hununua bidhaa na chakula, sasa wafanyabiashara hawaruhusiwi kufika eneo hilo, kutokana na miongozo iliyopo ya kupambana na Covid -19.

**BBC**



Kiongozi wa Chama cha Yamina, Naftali Bennett (kushoto), akiteta jambo wakati akizungumza na Yair Lapid ambaye ni kiongozi wa Chama cha Yesh Atid, katika kikao maalum wa wabunge kumchagua rais mpya, Knesset, kwenye bunge la Israeli, Jerusalem juzi. Viongozi hao wanatarajia kuungana kuanzisha serikali ya upinzani. **PICHA: AP**

# Wapinzani wa Netanyahu kuunda serikali

**Telaviv,** ISRAEL

VIONGOZI wa upinzani Israel, wametangaza kufikia makubalino ya kuunda serikali mpya ya mseto, hatua itakayofungua njia ya kumuondoa madarakani Waziri Mkuu wa muda mrefu wa nchi hiyo, Benjamin Netanyahu.

Tangazo hilo kutoka kwa kiongozi wa upinzani, Yair Lapid na mshirika wake Naftali Bennett, lilitolewa muda mfupi kabla ya saa sita usiku wa kuamkia jana na kufanikisha kuzuia Israel kuingia kwenye uchaguzi wa tano, ndani ya kipindi cha miaka miwili.

Lapid aliandika kupitia ukurasa wa Twitter kuwa, serikali hiyo mpya itafanya kazi kwa ajili ya raia wote wa Israel na itafanya kila linalowezekana kuwaunganisha watu wa taifa hilo.

Jumapili iliyopita Lapid, mtangazaji wa zamani wa televisheni anayeongoza chama cha siasa za wastani cha Yesh Atid, alipata uungaji mkono muhimu kutoka kwa Bennett, ambaye ni kiongozi wa chama mrengo wa kulia cha Yamina.

Chini ya makubaliano yaliyofikiwa, Lapid na mshirika wake Bennett, watapokezana wadhifa wa Waziri Mkuu kwa Benett kuhudumu kwa miaka miwili ya mwanzo, na Lapid ataongoza miaka miwili ya mwisho ya muhula wa miaka minne.

Hata hivyo, makubaliano hayo yatahitaji kwanza kuthibitishwa na bunge la nchi hiyo, Knesset katika kura inayotarajiwa wiki ijayo.

Iwapo hatua hiyo itapitishwa Lapid na washirika wake, watafanikiwa kumaliza enzi ya Benjamin Netanyahu madarakani, ambaye amekuwa waziri mkuu wa Israel kwa miaka 12.

Netanyahu, ambaye anapambana kufa na kupona kubakia madarakani wakati akikabiliwa na kesi ya rushwa, anatarajiwa kufanya kila awezalo katika siku zinazokuja kuhakikisha muungano huo mpya hautachukua mamlaka.

Wafuasi wa Netanyahu na Upinzani wapigana vijembe.

Tangazo la kupatikana makubaliano ya kuundwa serikali, limezusha hisia mseto na hata vita vya maneno, kati ya wafuasi wa Netanyahu na wale wanaounga mkono upande wa upinzani.

Waandamanaji kutoka pande zote mbili walikusanyika katikati ya mji mkuu wa Israel, ambako viongozi wa upinzani walikuwa wakifanya majadiliano ya kuunda serikali ya pamoja.

Mmoja ya wafuasi wa upinzani alisema "Sisi ndiyo washindi rafiki yangu. Sisi ni washindi. Tunashinda. Tumeshinda pambano hili. Tulishinda uchaguzi. Hatimaye tumepata serikali."

Hata hivyo wafuasi wa Netanyahu nao hawakuwa nyuma kumpigia debe mwanasiasa huyo na kufanya kejeli kuwa muungano wa upinzani hautavuka vigingi.

"Wiki moja na nusu ijayo hakutakuwa na serikali iliyopigiwa kura kwenye Knesset. Zingatia maneno yangu ninakwambia wiki moja na nusu baadaye hakutakuwa na serikali. Watapambana wenyewe kwa wenyewe na hakutakuwa na serikali." alisema mfuasi wa Netanyahu.

Katika uchaguzi wa Machi, mwaka huu, chama cha Netanyahu cha Likud, kilipata wingi wa viti bungeni, ingawa idadi haikutosha kumwezesha kuunda serikali na washirika wake wa vyama vidogo walikataa kuungana kupata wingi ndani ya Bunge.

**DW**

# Wazazi wafariki watoto wakitekwa Nigeria

**Tegina,** NIGERIA

WAZAZI wawili wa watoto wa shule waliotekwa nyara katika eneo la katika jimbo la kati la Nigeria la Niger, wamekufa kutokana na mshtuko, vimesema vyombo vya habari.

Walipatwa na mshtuko baada ya magenge kuwateka wanafunzi kutoka kwenye shule yao Jumapili, wiki iliyopita.

Wazazi hao walisemekana waliugua ghafla na kupoteza fahamu.

Watekaji nyara wanasemekana kuwa wamekuwa wakiwaomba kikombozi kabla ya kuwachilia watoto wao na wametishia maisha yao, iwapo hawatalipwa, kulingana na taarifa.

Awali, Mkuu wa shule ya kiislamu aliiambia BBC kwamba, alizungumza na watekaji nyara na wakamuhakikishia kuwa watoto walikuwa wazima na wenye afya.

Abubakar Alhassan alisema kuwa, wanafunzi 136 hawajulikani walipo, wakiwamo watoto wake watano, baada ya kuhesabu idadi ya watoto kufuatia utekaji huo.

Walimu watatu pia hawajulikani walipo.

Hata hivyo, bado hakuna taarifa rasmi ya idadi kamili ya wanafunzi waliotekwa nyara.

**BBC**

# Bensouda aita washukiwa wa uhalifu kivita Darfur

**Khartoum,** SUDAN

MWENDESHA Mashtaka Mkuu wa Mahakama ya Kimataifa ya ICC, Fatou Bensouda ambaye amekuwa ziarani nchini Sudan, ametoa wito kwa serikali nchini humo, kusaidia kumfikisha Ahmed Haroun, mahakamani kujibu mashtaka ya uhalifu wa kivita katika jimbo la Darfur.

Haroun, ni miongoni mwa washukiwa wanaotakiwa na ICC pamoja na rais wa zamani, Omar al-Bashir na kiongozi wa kundi la Janjaweed Abd-Al-Rahman ambaye alijiwasilisha kwenye Mahakama hiyo mwaka uliopita.

Bensuda alisema ana uhakika majaji wa ICC, watathibitisha mashtaka dhidi ya Ahmed Haroun.

"Ukianza na mfano wa Ahmed Haroun, ambaye nilichukua muda kuelezea kuwa majaji wanaosikiliza kesi ya kuthibitisha mashtaka, wanatarajiwa kutoa uamuzi wao kufikia mwisho wa mwezi wa Julai, kuamua iwapo mashtaka yatathitibitishwa au la.

"Tuna uhakika kuwa kwa namna tumewasilisha kesi yetu, tunaamini kuwa mashataka hayo yatathibitishwa".

**RFI**

# ANCELOTTI

## ATAMANI KUENDELEA KUMNOA RAMOS




**MADRID, Hispania**

CARLO Ancelotti anataka kumfundisha, Sergio Ramos katika msimu ujao, lakini kocha huyo mpya wa Real Madrid anatambua kwamba majaliwa ya beki huyo mkongwe bado hayajulikani.

Mkataba wa Ramos unamalizika mwishoni mwa mwezi huu na hakuna mazungumzo yoyote juu ya kumwongezea mkataba mpya.

Licha ya muda mwingi wa msimu wa 2020-21 alikumbwa na majeruhi na kugharimu nafasi yake kwenye michuano ya Euro 2020 kwa kutoitwa katika kikosi cha Hispania, lakini beki huyo mwenye umri wa miaka 35 alithibitisha uwezo wake dimbani.

Kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga, alikuwa na asilimia 80 ya ukabaji mzuri na kumfanya kuwa mchezaji aliyekaba zaidi kuliko yoyote wa Real Madrid.

Huku Ancelotti akiwa amejiunga tena na Madrid Jumanne akitoka kwa miamba wa Ligi Kuu England, Everton, hana uhakika kuhusu majaliwa ya Ramos.

Lakini kocha huyo raia wa Italia ameweka wazi kwamba, angependa kumnoa Ramos msimu ujao hapo katika dimba la Santiago Bernabeu ambako awali alifanya kazi ya mwaka 2013 na 2015.

"Sergio Ramos ni mchezaji muhimu kwa Real Madrid; amekuwa mchezaji muhimu sana na tunajaribu kuzungumza naye," alisema Anceloti akiwaambia waandishi wa habari Jumatano.




## MBAPPE KUPISHANA NA RONALDO PSG

**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappe anaweza kujiunga na Real Madrid na inaweza kushuhudiwa Cristiano Ronaldo akiondoka Juventus na kwenda Paris Saint-Germain, kwa mujibu wa Gazzetta dello Sport.

Majaliwa ya Mbappe yametawala vichwa vya vyombo vya habari kwa muda mrefu sasa.

Nyota huyo wa Paris Saint-Germain amekuwa akiwaniwa na Real Madrid kwa muda mrefu sana.

Na sasa Mbappe anatajwa atajiunga na Madrid kipindi hiki cha majira ya joto, huku Ronaldo akienda kuchukua nafasi yake kule PSG.

Ronaldo mapema wiki iliyopita aliripotiwa kuwaaga wachezaji wenzake kule Juventus na kuna uwezekano akandoka kwa kibibi kizee hicho cha Turin kipindi hiki cha majira ya joto.

## MORATA HAJUI MAJALIWA YAKE JUVE

**MADRID, Hispania**

ALVARO Morata amesema hajui ataichezea timu gani msimu ujao huku kukiwa na uvumi kwamba straika huyo wa Hispania anapanga kuongeza muda wa kukaa Juventus.

Morata alirudi Juve kwa mkopo akitokea Atletico Madrid kwa msimu huu wa 2020-21.

Miamba hao wa Serie A wanakipengele cha kumrudisha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 hapo Turin kwa msimu wa 2021-22 kwa mkopo au kumsajili kwa mkataba wa kudumu kwenye thamani ya euro milioni 45.

Imeripotiwa kwamba Morata atarudi kwa mkopo hapo Bianconeri kuanza maisha mapya na kocha mpya, Massimiliano Allegri, ambaye amechukua nafasi ya Andrea Pirlo.

Bado hakuna habari mpya kuhusu mchezaji huyo wa zamani wa Real Madrid na Chelsea, Morata wakati akijiandaa kuiwakilisha Hispania kwenye michuano ya Euro 2020.

Alipoulizwa kuhusu majaliwa yake, aliiambia Radio MARCA: "Sijui. Nipo hapa. Wakala wangu (Juanma) ndio anajua kila kitu.

"Sina habari yoyote na kesho atanipigia simu na kusema: Unatakiwa kucheza hapa'. Tuna nyumba Madrid na kulikuwa na wakati mzuri sana."

Morata alifunga mabao 20 kwenye mechi 44 za mechi zote akiwa na Juve ambayo ilimaliza nafasi ya nne kwenye Serie A.

## HABARI MICHEZO



# INZAGHI
## ACHUKUA MIKOBA INTER

**MILAN, Italia**

KOCHA wa Lazio, Simone Inzaghi yuko tayari kutua Inter Milan baada ya Antonio Conte kuachana na klabu hiyo.

Makubaliano hayo yanapaswa kukamilika baada ya Inzaghi kuamua kukataa pendekezo la mkataba mpya alilopewa na Lazio.

Inzaghi atasaini mkataba na Inter hadi Juni, mwaka 2023 kama ilivyotangazwa na klabu hiyo kupitia kwenye tovuti yake.

Awali Maurizio Sarri, Paulo Fonseca, Sinisa Mihajlovic na Sergio Conceiçao walikuwa wanatajwa kuchukua mikoba ya Conte hapo Inter Milan.

Conte ataamua maisha yake ya baadaye mara tu baada ya kuondoka Inter, klabu nyingi zinavutiwa na huduma yake huku Tottenham wakiongoza mbio hizo.

Simone atakuwa kocha wa mpya wa Inter, makubaliano ya miaka miwili tayari yameshafikiwa na atasaini katika masaa machache yajayo.

## DE BRUYNE KUIKOSA URUSI

**LONDON, England**

KEVIN De Bruyne anaweza kukosa kuichezea Ubelgiji katika mchezo wa ufunguzi wa michuano ya Euro 2020 dhidi ya Urusi utakaochezwa Juni 12, mwaka huu, amesema kocha Roberto Martinez.

De Bruyne aliumia baada ya kugongana na mlinzi wa Chelsea, Antonio Rudiger kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyochezwa Jumamosi iliyopita.

Kiungo huyo hahitaji upasuaji, lakini Martinez hana uhakika kama mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 atakuwa fiti kwenye mchezo huo wa ufunguzi.

"Sina uhakika kama De Bruyne atakuwa fiti kwa mchezo wa kwanza," alisema Martinez akiwaambia waandishi wa habari Jumatano.

"Tulifanya uamuzi kuhusu yeye, lakini sina uhakika kabisa kama atakuwa fiti kwenye mchezo huu.

"Naweza kusema kwamba, baada ya wiki moja anaweza kuwa fiti, lakini sio sasa, kwani bado anauguza majeruhi.

"Anaweza kuwa kwenye michuano ya Euro, lakini sio kwa sasa, maana ufiti wake bado ni tatizo."

## BARCA, UNITED ZAMWANIA MORENO

**MANCHESTER, England**

NYOTA wa Villarreal, Gerard Moreno, amekuwa kwenye rada za Manchester United pamoja na Barcelona ambao wote wanataka huduma yake, kwa mujibu wa jarida la Fichajes.

Katika mechi 46 alizocheza Villarreal, Moreno alifanikisha kufunga mabao 30, kitu kilichomfanya kuwa miongoni mwa mastraika bora Ulaya msimu huu.

Uchezaji wa Moreno umeshangaza watu wengi na imesababisha klabu ya Barcelona na United kutaka saini yake.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, anawindwa na klabu hizi na inatarajiwa wakati wowote timu yake itapewa ofa ya mchezaji huyu.

Bado haijatajwa Villarreal watahitaji kiasi gani, lakini kwa uwezo aliouonyesha msimu huu, bila shaka atakuwa na thamani kubwa sana. Barcelona wamesajili Sergio Aguero hivi karibuni, lakini Moreno atakuwa ongezo lingine muhimu katika kikosi hicho cha Barca.

Kwa upande wa United, kuongeza kwa mkataba kwa Edinson Cavani ni muhimu lakini kutokana na umri wake, hawezi kucheza kila mechi na Moreno atakuwa muhimu sana klabuni hapo.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# LUKAKU AKATAA KUONDOKA MILAN

## Ni baada ya kuwapo kwa tetesi za kutakiwa na Madrid, Barca na Chelsea huku...

**MILAN,** Italia

NYOTA wa Inter Milan, Romelu Lukaku, amesisitiza anabakia kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu Italia, Serie A, huku kukiwa na uvumi kuhusu majaliwa yake klabuni hapo.

Lukaku amekuwa akihusishwa na mpango wa kutimka Inter baada ya kuondoka kwa kocha, Antonio Conte wakati Nerazzurri hao wakiwa kwenye wakati mgumu kutokana na matatizo ya kifedha yaliyosababishwa na mlipuko wa virusi vya corona.

Licha ya kuiongoza Inter Milan kwenye taji lake la kwanza la Ligi Kuu Italia, Scudetto, kwa kipindi cha mwongo mmoja, Lukaku ameripotiwa kuwaniwa na Chelsea, Real Madrid na Barcelona.

Hata hivyo, Lukaku hana mpango wa kuondoka hapo kwenye dimba la San Siro kwani ana malengo ya kutaka kutwaa taji jingine na Inter baada ya kutajwa kuwa mchezaji bora wa msimu huu.

"Nabakia Inter," amesema Lukaku - ambaye aliwasili hapo kutoka Manchester United mwaka 2019 - akiambia VTM wakati Inter ikiripotiwa kujiandaa kumteua kocha wa zamani wa Lazio, Simone Inzaghi.

"Tayari nimezungumza na mtu huyu anayekuja kuwa kocha wetu mpya. Pengine sikutakiwa kusema hivyo mapema... lakini yalikuwa majadiliano mazuri sana.

"Changamoto ni kushinda tena. Najisikia vizuri hapa, hatimaye nimeshinda taji.

> **"Kwa hakika nili furahi sana, lakini nataka kushinda tena hapa San Siro."**

Lukaku alifunga mabao 24 katika mechi 36 za ligi alizocheza msimu huu wa 2020-21, huku fowadi huyo wa Ubelgiji akitoa pasi za mwisho 11.

## KWA UFUPI

### MADRID KUMSAJILI MBAPPE

REAL Madrid watamsajili mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 22, anayekipiga Paris St-Germain. (***La Gazzetta dello Sport,via Mail***)

### MOURINHO ALITAJWA

JOSE Mourinho aliwasiliana na Real Madrid wiki iliyopita, kabla ya kumteua Carlo Anclotti kuwa kocha wa klabu hiyo, pamoja na kocha huyo wa zamani wa Real na Tottenham kukubali kutua Roma mwezi uliopita. (***Telegraph***)

### CHELSEA YAKWAMA

MATUMAINI ya Chelsea ya kupata saini ya Romelu Lukaku yamegonga mwamba baada ya mchezaji huyo mwenye umri wamiaka 28, kusema kuwa anasalia Inter Milan. (***Football Italia***)

### BARCA, DEPAY WATETA

BARCELONA bado wako kwenye mazungumzo na mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Memphis Depay (27), kuhusu uhamisho wa bure kutoka Lyon.

### WIJNALDUM KIMEELEWEKA

NYOTA wa Liverpool, Georginio Wijnaldum mwenye umri wa miaka 30, atajiunga na Barcelona kwa uhamisho wa bure wiki ijayo. (***Fabrizio Romano,Twitter***)

### TRIPPER ANUKIA UNITED

MANCHESTER United wamerejesha nia yao ya kumsajili beki wa kulia, Kieran Trippier mwenye umri wa miaka 30, kutoka Atletico Madrid. (***Manchester Evening News***)

### VILLA YAMTAKA WOOD

ASTON Villa ni moja kati ya klabu 12 za Ligi Kuu England zinazopanga uhamisho wa mshambuliaji, Chris Wood na Burnley, itataka takribani pauni milioni 30 kwa ajili ya kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29. (***Football Insider***)

### GIROUD SOKONI RASMI

KLABU za West Ham na New York City zimetangaza ofa kwa mshambuliaji wa Ufaransa, Olivier Giroud mwenye umri wa miaka 34, ambaye anajiandaa kuondoka Chelsea kwa uhamisho huru.(***Calciomercato***)

### HAZARD, BALE SAFI

KOCHA mpya wa Real Madrid, Carlos Ancelotti amesema mshambuliaji wa Wales, Gareth Bale mwenye umri wa miaka 31 na mshambuliaji wa Ubelgiji, Eden Hazard (30), bado wanaweza kubakia klabuni hapo. (***Guardian***)

### NEUHAUS AIKANA BAYERN

KUNGO wa kati wa Borussia Monchengladbach, Florian Neuhaus mwenye umri wa miaka 24, ambaye amekuwa akihusishwa na Liverpool amekana taarifa kuwa amefikia makubaliano ya kujiunga na Bayern Munich. (***Tageszeitung***)

### UNITED, SPURS VITANI

ARSENAL, Manchester United na Totteham Hotspur zote zimeonyesha nia ya kumtaka beki wa kulia wa Lille, Zeki Celik mwenye umri wa miaka 24. (***Standard***)

HABARI MICHEZO

## TAMASHA LA STARA KUFANYIKA JULAI

**Na Mwandishi Wetu**

ZAIDI ya wabunifu 20 kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini wanatarajia kushiriki katika tamasha la saba la Wiki ya Mitindo ya Stara ambalo limepangwa kufanyika Julai 30 na 31, mwaka huu jijini Dar es Salaam huku likiwa na kauli mbiu ya 'Uhuru'.

Mbali na maonyesho ya jukwaani, pia kutakuwa na vibanda vya wabunifu watakaoonyesha bidhaa kwa ajili ya wateja watakaohitaji kuzinunua.

Mwanzilishi wa onyesho hilo, Latifah Makau aliliambia gazeti hili kwa sasa wanaendelea na semina na mikutano ya awali kwa ajili ya kuwatayarisha wabunifu watakaoshiriki kujiandaa kwa weledi.

"Katika jitahada zetu za kuunga mkono nguvu ya mitindo kushawishi, tulifikiri itakuwa busara kutumia jukwaa letu kukuza uelewa wa mambo mbalimbali na labda kuanza kuleta mabadiliko ambayo tunataka kuyaona," alisema Latifah.Aliongeza kutumia neno Uhuru ni dhana ya fimbo ya kina kwenye soko.

Alisema pia washiriki watapata fursa ya kukutana na washawishi katika tasnia ya mitindo, watu mashuhuri katika ulimwengu wa mitindo ya kawaida wakati wawekezaji watapata nafasi ya kuungana na masoko mapya.

"Tunatoa mwongozo wa kufundisha na kuwanoa wanamitindo na wabunifu," Latifah alisema na kuongeza maonyesho hayo pia yatajumuisha sanaa ya hina na mapishi.

## POLISI YAIPANIA KVZ LALA SALAMA

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BENCHI la ufundi la Polisi limesema litapambana kuhakikisha timu yao inapata matokeo chanya katika mechi ya mwisho ya Ligi Kuu Zanzibar dhidi ya KVZ ili kujiepusha na janga la kushuka daraja.

Polisi yenye pointi 24, iko katika nafasi ya tatu kutoka chini kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 12, inahitaji ushindi tu ili kujinusuru na panga hilo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Polisi, Yusuph Sape alisema amewataka wachezaji wake kuongeza umakini na kufuata maelekezo kikamilifu ili wakahakikishe wanaondoka na pointi tatu katika mchezo huo muhimu kwao. Sape alisema timu yao iko katika nafasi mbaya na hivyo wanatakiwa kuongeza juhudi ili watimize malengo ya kubakia kwenye ligi hiyo baada ya kukiri walikuwa na wakati mbaya katika msimu huu.

"Tuko katika nafasi ya hatari ya kushuka, kubaki kwetu kwenye Ligi Kuu kutaangalia pia na matokeo ya mpinzani wetu Chuoni ambaye ana pointi 23, tunawaombea dua mbaya wapinzani katika mechi zao zilizobakia," alisema Sape.

# KIKWETE AZINDUA UWANJA WA KIKAPU, ATEMA CHECHE

**Na Faustine Feliciane**

RAIS Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Jakaya Kikwete, amezindua mradi wa ujenzi wa uwanja wa mpira wa kikapu kwenye Shule ya Sekondari Minaki iliyopo katika Wilaya ya Kisarawe na kutoa wito kwa Shirikisho la mchezo huo nchini (TBF), kuweka mkazo kufundisha walimu.

Mradi huo unajengwa kwa msaada wa Taasisi ya GOA (Giant of Africa), ambayo inaongozwa na Rais wa klabu ya Toronto Raptors inayoshiriki Ligi ya NBA ya Marekani, Masai Ujiri.

Kikwete alisema mpira wa kikapu hapa nchini utapiga hatua kama kutakua na miundo mbinu mizuri pamoja na walimu wa kufundisha vijana kuufahamu vyema mchezo huo.

"Niwaombe Wana-Kisarawe kukitunze kiwanja hiki pindi kitakapomalizika, kwa sabau uwepo wa kiwanja hiki ni hatua moja zaidi katika kuleta maendeleo ya mchezo huu ambao mimi mwenyewe nimeucheza miaka ya nyuma," alisema Kikwete.

Alisema Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo amefanya kazi kubwa kuwashawishi GOA na TBF kuleta mradi huo wa uwanja wilayani huko ili kuchangia kukuza na kuendeleza vipaji vya vijana.

"Viwanja hivi nimeambiwa vinajengwa na sehemu nyingi Afrika, lakini katika hivyo kimoja kinajengwa Tanzania na ndio hiki pekee, hii ni kazi kubwa imefanywa na Mkuu wa Wilaya (Jokate), ni jukumu letu kukitunza ili kisaidie kuinua mchezo huu," Kikwete alisema.

Pia ameitaka TBF kuandaa mapema timu za vijana zitakazoshiriki mashindano ya Afrika yanayotarajiwa kufanyika ifikapo Agosti, mwaka huu huko Mali ili ziende kufanya vizuri na kuepuka lawama na kufanya maandalizi ya zimamoto.

"Lakini pia niwaombe wenzetu wa GOA kama ambavyo wametusaidia kwenye kiwanja hiki, watusaidie pia katika kutoa mafunzo ya ufundishaji mchezo huu kwa walimu ambao watawafundisha vijana wetu mashuleni," aliongeza Kikwete.

**Naye Mkuu wa Shule ya Minaki, Harold Chungu, alishukuru ujenzi wa uwanja huo kuwepo shuleni kwake.**

Kwa upande wake Mkandarasi wa uwanja huo, Josephat Abraham kutoka Kenya alisema kama kutakuwa na hali nzuri ya hewa , ujenzi huo utakamilika baada ya miezi mitatu kuanzia leo ambapo wanatarajia kuanza rasmi ujenzi.



Mratibu wa mchezo wa rede, Chairu Nyamwija (kulia), akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya fainali ya mashindano ya mchezo huo zitakazofanyika kesho kwenye Uwanja wa Shule ya Msingi Hananasifu jijini Dar es Salaam. Kushoto ni Diwani wa Kata ya Hananasifu, Wilfred Ntamwija. PICHA: MIRAJI MSALA

# Yanga, Lamine sasa kimeeleweka

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuwapo kwa mgongano kati ya nahodha wa Yanga, Lamine Moro na Kocha Mkuu, Nasreddine Nabi, beki huyo wa kimataifa kutoka Ghana ameungana na wachezaji wenzake katika kambi ya timu hiyo kuendelea na maandalizi ya mechi za Ligi Kuu Bara zilizobakia kufuatia makubaliano yaliyofikiwa kati ya pande mbili hizo, imeelezwa.

Awali ilielezwa Lamine amesimamishwa kwa muda usiojulikana na Nabi baada ya kuwapo kwa vitendo vya utovu wa nidhamu, jambo ambalo beki huyo alilikataa na kuutaka uongozi uweke taarifa sahihi juu yake.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kaimu Katibu Mkuu wa Yanga, Haji Mfikirwa alisema baada ya nyota huyo kusimamishwa, viongozi walikutana na Nabi pamoja na mchezaji huyo kwa lengo la kusikiliza hoja za kila upande na hatimaye kuweka mambo sawa.

Mfikirwa alisema uongozi ulilazimika kulifanyia kazi suala hilo kwa sababu linahitaji kuona kila mchezaji anafuata taratibu na kanuni za klabu hiyo kikamilifu.

"Tulisikiliza hoja za pande zote mbili, tulikutana na Lamine wakati timu mkoani, baadaye tukazungumza na kocha (Nabi), hivyo tumefanyia kazi hoja zao na sasa mambo safi na Lamine yuko kambini Avic Town, Kigamboni, akiendelea na mazoezi kwa ajili ya michezo yetu ijayo," alisema Mfikirwa.

Kutokana na adhabu aliyokuwa anaitumikia, Lamine alikosa mechi mbili za Ligi Kuu Bara dhidi ya Namungo FC na JKT Tanzania pamoja na mchezo wa hatua ya robo fainali mashindano ya Kombe la FA dhidi ya Mwadui.

Michezo
Ijumaa Juni 4, 2021
Nipashe



LUKAKU AKATAA KUONDOKA MILAN

HABARI UK 22




Winga wa kimataifa wa Simba, Luis Miquissone (kushoto), akijipanga kupiga mpira mbele ya beki wa kati wa Ruvu Shooting, Zuberi Dabi (kulia), katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza jana. Simba ilishinda mabao 3-0. **PICHA: SIMBA SC**

# SIMBA HAIKAMATIKI

## ●●●Yapata ushindi wa sita mfululizo,Ndugai atamba sasa ni mwendo wa tatu tatu...

**Na Adam Fungamwango**

MABAO mawili ya nahodha wa Simba, John Bocco katika ushindi wa magoli 3-0 dhidi ya Ruvu Shooting yaliwafanya mabingwa hao watetezi kuendelea kujiimarisha kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu ambao unaelekea ukingoni.

Hata hivyo wenyeji Ruvu Shooting ambao jana waliuteua Uwanja wa CCM Kirumba kuwa nyumbani ilipoteza wachezaji wawili dakika za mwisho kwa kuonyeshwa kadi nyekundu.

Nahodha wa Wekundu wa Msimbazi, Bocco, sasa amefikisha mabao 13, moja nyuma ya kinara wa mabao kwenye ligi hiyo, mshambuliaji wa Azam FC, Prince Dube ambaye ametikisa nyavu mara 14.

Bocco amefunga mabao saba katika mechi nne mfululizo ambazo amecheza. Mabao mawili alifunga kwenye mechi dhidi ya Kaizer Chiefs kwenye michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa, mawili kwenye mechi ya Kombe la FA dhidi ya Dodoma Jiji, moja dhidi ya Namungo katika mechi nyingine ya kiporo.

Kwenye mechi hiyo, Ruvu Shooting ilianza kucheza pungufu kuanzia dakika ya 71, baada ya Juma Nyosso kumpiga ngumi beki wa Simba, Shomari Kapombe huku dakika tatu kabla mechi kumalizika, golikipa Abdallah Rashid naye alizawadiwa kadi nyekundu na mwamuzi, Emmanuel Mwandembwa kwa kumwangusha, Bernard Morrison ndani ya eneo la hatari na kusababisha penalti iliyoipatia Simba bao la tatu.

Rally Bwalya, nusura alipatie Simba bao lingine akiwa katika eneo la hatari baada ya kuachia kombora kali la juu, lakini kipa Rashid aliruka na kuupiga ngumi mpira huo, ukatoka nje ya kuwa kona ambayo ndiyo iliyozaa bao.

Alikuwa ni Bocco dakika ya 17, aliyefunga kona hiyo fupi iliyopigwa na Bwalya kwa Miquissone ambaye alipiga krosi ya chini iliyoguswa na mfungaji na kumpoteza maboya kipa, ukajaa wavuni.

Edward Charles alimshughulisha Manula dakika ya 28, akiwa umbali ya mita 35 hivi, aliachia mkwaju mkali ambao kipa wa Simba aliruka juu kama nyani na kuukamata.

Kipindi cha pili Ruvu ilianza mechi hiyo kwa kasi na kufanya mashabulizi makali kwenye lango la Simba, lakini ilijikuta ikifunga bao lililotokana na shambulio la kushtukiza.

Alikuwa ni Morrison aliyeingia kuchukua nafasi ya Hassan Dilunga, aliyepata pasi ndefu akakimbia nayo kabla ya kupiga krosi iliyomkuta Chris Mugalu dakika ya 61, akaujaza wavuni na kuifungia Simba bao la pili.

Kuingia kwa bao hilo kulionekana kuwachanganya wachezaji wa Ruvu Shooting na kuanza kucheza kwa kutumia nguvu zaidi kuliko akili kiasi cha kufanya makosa mengi yaliyowagharimu.

Kadi nyekundu ya Nyosso, ilisababisha Kocha, Boniface Mkwasa, kumtoa Zuberi Dabi na kumwingiza, Frank Ikobela ili kuongeza nguvu, lakini haikusaidia hadi iliporuhusu bao la tatu.

Alikuwa ni Morrison tena alipompiga chenga ya kifua kipa, Rashid kabla ya kumwangusha na kusababisha kadi hiyo iliyosababisha penalti ambayo ilifungwa na Bocco, golini akiwa kipa mwingine chaguo la pili, Bidii Hussein.

Kwa matokeo hayo, Simba sasa imefikisha ya pointi 67, ikiwa bado ina viporo viwili mkononi ikifuatiwa na Yanga yenye pointi pointi 61 baada ya kucheza mechi 29.

Wakati huo huo Spika wa Bunge, Job Ndungai, amesema sasa hivi ni mwendo wa tatu tatu kuelekea Julai 3, mwaka huu ambapo watani wa jadi watakutana katika mechi ya kiporo ya Ligi Kuu Bara.

# YANGA SC UPEPO MBAYA WAVUMA

**Na Saada Akida**

BAADA ya kusambaa kwa video ikionyesha Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli akisema hawautambui mchezo wa watani wa jadi unaotarajiwa kufanyika Julai 3, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, uongozi wa klabu hiyo umesema unaheshimu ratiba mpya iliyotolewa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

Bumbuli amenukuliwa akisema Yanga ikajiandaa na mechi nne tu za Ligi Kuu Tanzania Bara ambazo ni dhidi ya Ruvu Shooting itakayochezwa Juni 17, Mwadui FC (Juni 20), Ihefu (Julai 14) na Dodoma Jiji itakayofanyika Julai 18 ambayo ni siku ya funga pazia.

Kaimu Katibu Mkuu wa Yanga, Haji Mfikirwa aliliambia gazeti hili jana klabu yao inaheshimu makubaliano yaliyofikiwa katika kikao cha mwisho walichokutana wakiwamo viongozi wa Serikali, TFF na Bodi ya Ligi.

Mfikirwa alisema kauli hiyo iliyotolewa na Bumbuli haikuwa rasmi na kusisitiza Yanga inaheshimu ratiba ambayo imetolewa na itaifuata.

"Viongozi hatujatoa tamko lolote kuhusu mchezo wetu dhidi ya Simba, tunaheshimu ratiba iliyopangwa na Bodi ya Ligi na TFF, aliyoyasema Ofisa Habari wetu yasipewe kipaumbele kwa sababu ameongea kama ilivyo kwa mashabiki na makomandoo wengine," alisema Mfikirwa.

Kiongozi huyo alisema bado wanaendelea na vikao vya ndani kwa ajili ya kuweka mipango ya mechi zao zilizobakia ikiwamo mchezo huo wa watani wa jadi na mtanange wa hatua ya nusu fainali ya Kombe la FA ambao watakutana na Biashara United.

Aliwataka mashabiki wao kuendelea kusubiri tamko rasmi la klabu ambayo imedhamiria kuhakikisha timu hiyo inafanya vizuri katika michezo yote iliyopo mbele yao.

"Jumatatu (wiki hii), wachezaji wote waliingia kuendelea na maandalizi ya mechi zetu hizo, kasoro nyota wawili ambao ni Sogne Yacouba na Mukoko Tonombe ambao wameondoka kwenda kujiunga na timu zao za Taifa," alisema Mfikirwa.

Aliongeza benchi la ufundi limependekeza kupata mechi tatu za kirafiki na Jumapili wataanza kucheza dhidi ya African Lyon kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002